Sauti Isiyojulikana

Asante, Ndugu.

2 Hebu tuendelee kusimama, kwa muda kidogo tu, kwa ajili ya maombi, na tuinamishe vichwa vyetu. Kunaweza kukawa na haja sasa? Inua mkono wako, naye Mungu atakuona, nina hakika. Moyoni mwako tu sema, "Nikumbuke, Bwana, nina ninii *fulani*, *kama* . . . "

3 Baba yetu wa Mbinguni, tunakushukuru tunapokaribia Kiti Chako cha neema tukiwa na shukrani moyoni mwetu, milele tukiokoa nafsi zetu kutoka kwenye maeneo yaliyopotea ya waliolaaniwa. Nasi tunakushukuru ya kwamba, kwa neema ya Mungu, sisi ni watoto Wako, usiku wa leo.

4 Ninaomba kwa ajili ya kila moja ya haja hizi, Baba. Mkono wangu uko juu pia, Mungu, Kwako, nina haja. Haja yangu, usiku wa leo, Baba, ni kuifanya ijulikane, wakati wanapofanya zao zijulikane, kwa njia yao wenyewe ya kuomba, Mungu, yangu ni kwamba utaokoa kila nafsi iliyopotea hapa ndani, usiku wa leo, kwamba utamponya kila mgonjwa, kwamba utamjaza kila mwaminio na Roho Mtakatifu.

5 Njoo kwetu, Bwana Yesu, tunakuhitaji, tunakungojea Wewe. Na tunapoendelea kungojea, tunajikabidhi mikononi Mwako, fanya nasi upendavyo. Kwa kuwa tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

6 Mwaweza kuketi. Kuna . . . Nina furaha sana kurudi tena, usiku wa leo, kanisani na kuwa katika huduma ya Bwana Mungu, na tukitumaini ya kwamba huu utakuwa ndio usiku ambao Bwana atapata sifa kwa lolote lililo kusudi la kukusanyika kwetu, usiku wa leo. Alisema, "Neno langu halitanirudia bure, Litatimiza yale liliyokusudiwa," nasi tunajua litafanya hivyo.

7 Mchungaji alikuwa tu akiniambia juu ya msichana mdogo aliyeketi *hapa* nyuma, alikuwa kwenye mkutano usiku ule ule ambao binti wa Ndugu Bryant Mitchell na mkwe wake waliitwa. Naye maskini msichana huyu aliitwa kutoka kwenye kusanyiko akiwa na, aina fulani ya upele usoni mwake, aliponywa mara moja na angali mzima. Ninaamini ni maskini yule msichana aliyeketi . . . Huyo ni wewe? Naam. Nadhani mumempa nafasi ya kushuhudia. Simama, Mpenzi, tafadhali. Huyo, si ni msichana mdogo anayeonekana wa kupendeza? Hakuna upele usoni mwake sasa, kwa sababu kwamba—kwamba Yesu Kristo alimponya. Tuna furaha sana kwa hilo.

8 Na sasa, sitaki kuwaweka zaidi ya saa saba, kama ninaweza kuzuia. Hilo si ni baya? Samahani. La, sisemi "Samahani," la,

hilo si sawa, mnaona, kwa sababu sijawahi kusema chochote bado ambacho niliwahi kuwazia kwamba itanilazimu kulighairi, kwa sababu nimejaribu kulisema kwa moyo wangu wote, kutoka kwenye Neno. Na—nami naninii . . . Nasikitika nawatesa watu wengi sana.

9 Ndugu yangu mpendwa alikuwa amekuja kuniona alasiri ya leo, na mapema nikaingia kwenye maombi, ndipo mke akaingia kisiri, hadi mlangoni nilipokuwa, wala hakuniita, kisha akarudi na kumwambia nilikuwa katika maombi, arudi tena baada ya kitambo kidogo, wala hakuja. Nami nilikuwa na wasiwasi kidogo, nilifikiri kwamba angeninii . . . hakika angeelewa. Ndipo nikamwambia, "Ungeniita kwa vyovyote vile, wakati mojawapo wa hao ndugu alipopiga simu." Lakini kwa kawaida huniacha tu peke yangu, kwa sababu wakati mwingine maono hutokea pale, nami ninajua kitakachotukia kabla sijapata kufika kanisani. Mnaona? Mara nyingi imetokea huko.

10 Ninamtazama mtu sasa hivi, rafiki yangu mwema, Banks Wood. Wakati mvulana wake David . . . Ndugu Wood, pale, alikuwa Shahidi wa Yehova, mwanakandarasi, naye akamleta mvulana wake mkutanoni. Naye akamwona msichana usiku mmoja . . . Mnajua, Shahidi wa Yehova kidogo hupinga uponyaji wa Kiungu. Naye akashuka akaja, yeye na mkewe, alikuwa . . . walikuwa wa First Church Of God, Church Of God Mwenendo wa Anderson, kitu kama kanisa la Methodisti, nao wakashuka wakaja kwenye mkutano wa Louisville, ambapo tulikuwa tukiufanyia kwenye jumba la mikutano, jumba la mashambani.

11 Basi kulikuwa na msichana aliyegeuka kuwa jiwe, sijui ji—jina lake la matibabu sasa, lakini alikuwa katika hali mbaya sana, asingeweza kusogea kutoka kiunoni mwake kwenda chini. Katika saa chache baada ya kuombewa, alipanda na kushuka vipandio mbio na kila kitu, mzima kabisa.

12 Kwa hiyo, walikuwa na mvulana mwenye polio, naye mvulana huyo alikuwa na . . . Polio iliupinda mguu wake. Nami nikaenda ng'ambo baada ya hayo, ama, la, walienda Houston, Texas, yeye hakuingia. Nao walikuwa kule usiku ule Malaika wa Bwana, ile picha ilipopigwa.

13 Na jambo lingine, picha hizo ziko hapa sasa, na vitabu na kanda, huu ndio usiku wa mwisho wa kuzipata mkutanoni, maana hatuuzi Jumapili. Na kwa hivyo tuliweka sera ya kutouza Jumapili, unaweza kuwapa agizo lako, nao wanaweza kukutumia, lakini hatutaziuza.

14 Ndipo Bw. Wood akaleta . . . naye Bw. Wood akamleta mvulana wao, siwezi kupakumbuka mahali hapo huko Ohio karibu na ziwa kule, Columbus, naamini ndiko, Ohio. Hiyo ni kweli, Ndugu Banks? Ilikuwa . . . ? Cleveland, Cleveland, Cleveland, Ohio.

15 Basi kabla sijaja kwenye jengo hilo usiku ule, nilikuwa juu sana, yapata orofa kumi, nilikuwa nimeketi pale juu nikilia, Bw. Baxter akanijia, nyote mnamjua Ndugu Ern Baxter, nadhani, alikuwa hapa pamoja nami wakati uliopita, ndugu mzuri sana, basi akapanda akaja, nami nikasema, "Ni nini kinachonifanya kununa hivi?"

Akasema, "Usijisikie vibaya," akasema, akasema, "hata watu wakuu hujisikia hivyo." Hilo lilinifanya nijisikie vizuri basi.

16 Kwa hiyo usiku huo tuliposhuka, nilimwona mvulana mdogo aliyevaa jezi ya manjano, kitu kama sweta ndogo, aliyekuwa na polio, mguu wake umepindika, na akaponywa. Nikaendelea kuangalia kwenye kusanyiko, wala nisingeweza kuwaona. Ndipo hatimaye, naamini jinsi ilivyokuwa, Roho Mtakatifu aliwaita, nyuma kabisa nyuma ya jengo, na mahali fulani nyuma ya hema, ndivyo ilivyokuwa, ndipo mvulana huyo akaponywa papo hapo.

17 Huyo mtu akaiacha kazi yake ya ukandarasi, apate kuhamia huku, anaishi tu karibu nami sasa. Nao watu wake wote, karibu kila mmoja wao, wasomaji katika Mashahidi wa Yehova, kila mmoja wao amekuwa Mkristo aliyejazwa na Roho Mtakatifu.

18 David, sitaki kukufanya kitu cha kutazamwa. Je, uko hapa usiku wa leo, David? Simama. Mvulana huyo ameoa na ana watoto wawili. Hapo, hakika, ameketi hapo nyuma ya baba yake. Hapo alikuwepo yule mvulana ambaye alikuwa amelemazwa na polio kisha akaponywa.

19 Ninamkumbuka ndugu yake, sitaisahau kamwe, samahani, Ndugu Banks. Ndugu yake, mtu mzuri, na . . . lakini kwa namna fulani walimkana Ndugu Banks mara tu alipompokea Roho Mtakatifu. Walidhani aliingia wazimu, hakika.

20 Kwa hiyo, sasa, kama kuna Shahidi wa Yehova hapa, sio kuwadharau, mnaona, hata kidogo, ninaheshimu imani ya kila mtu. Hiyo ni kweli. Lakini hapo, mnaona, kuna uwezekano kwamba Mungu atakuita. Utaiona njia ya Bwana kikamilifu zaidi.

21 Kwa hiyo mtu huyu akaingia, naye kidogo aliudhika, mwajua, kwa ajili ya Banks, naye akaja pamoja na mtu mwingine, na kwa hiyo alitaka kujua huyu tapeli alikuwa nani.

Akasema, "Yuko *hapa* nje akikata nyasi."

22 Nanyi mnapaswa kuniona nikiwa nimestarehe kabisa, ndevu ndefu karibu *hivi*, na kofia kuu-kuu iliyoinama. Na mbona, nilihubiri na jamaa fulani miaka miwili ama mitatu, kisha nikakutana naye kwenye ziara ya mawindo, akasema, "Bwana, unaweza kuniambia mahali ninapoweza kumpata Kasisi Branham, huku juu?"

Nikasema, "Naamini ninaweza."

23 Vema, hapa si muda mrefu uliopita Kadilaka kubwa mno ilijongea hadi mlangoni, mwajua, na akasema . . . Nami nilikuwa na masharubu, na mchafu, na nilikuwa nikisafisha madirisha huko nje, naye huyo mtu akasema, "U hali gani, Bwana?" Kasema, "Unaweza kuniambia aliko Kasisi Branham sasa?"

Nikasema, "Yule ndiye mke wake pale *pale*, unaweza kumwuliza."

Naye nusura aanguke. Alinitazama, hakujua la kusema.

Kasema . . . Yeye . . . Yeye . . . Ikatokea tu alisema, "Mkutano wake unaofuata uko wapi?"

Naye akamwambia, naye akaondoka, akasema, "Loo, Bill!"

Nami nikasema . . .

24 Hivyo basi ndugu yake akasema . . . Nilikuwa nimeketi pale, naye Roho Mtakatifu akasema, "Yeye ni mtu aliyeoa, akamwacha mkewe, ana watoto wawili." Nikamwambia hilo.

25 Naye akamwangalia Banks, kana kwamba kusema Banks aliniambia. Mnaona, huyo ni ndugu yake hapa. Nilishika hilo upesi sana. Watu wananinii tu, hawatambui hilo. Mbona, bila shaka, Yeye hulifunua, mnaona. Wanaketi ndani ya vyumba . . .

26 Mara nyingi nimewafichua watu waliokuwa wakosoaji. Wakati mwingine . . . Hutaki kufanya hivyo, kwa vyovyote vile. Nilifanya hivyo wakati mmoja, mhudumu, mkosoaji sana, nami nikamwita, nikamwambia, nikasema, "Kwa nini ulifanya *hivi*, na *vile*, na *jambo fulani*." Jamani, akapoteza nusu ya kusanyiko lake, chochote kile. Kwa hivyo hilo—hilo si sawa. Mnaona, ninaliweka tu moyoni mwangu, naliachilia tu.

27 Lakini, hata hivyo, nikisimama pale nikalishika hilo, haingedhuru kumwambia, wakiwa wameketi pale wakati uo huo, nikasema, "Vema, huenda ikawa ulifikiri Banks aliniambia hilo. Lakini vipi kuhusu hivi majuzi usiku ulipokuwa pamoja na mwanamke fulani, mwenye nywele za kahawia? Ulikuwa umejifungia chumbani pamoja naye, ndipo mtu akagonga mlangoni, na hukuenda, ulichungulia dirishani. Ni jambo zuri, kichwa chako kingelipuliwa." Hilo lilimmaliza. Hiyo ni kweli. Alijua basi hiyo haikuwa . . . Banks hakuniambia hilo.

28 Ndipo baba yake akaja, ambaye alikuwa ni mmoja wa wasomaji, alikuwa anataka kuninyoosha kwelikweli kwa Maandiko. Sikumwambia chochote kamwe, tulikuwa tunaenda kwenye ziara ya kuvua samaki kesho yake, Bwana akasema nami, akasema, "Mwambie mambo yote yatakayotukia, yale hasa yatakayotukia, kwamba ni samaki wangapi watakamatwa, ni nani watakaowakamata na kila kitu, mrudi."

29 Nilipomwambia hayo, nilimwona akiangalia nyuma, kiajabu kidogo, akimwangalia Banks, akaangalia nyuma, na kuwaza, "Upuuzi." Lakini siku hiyo na usiku huo kila kitu kilitendeka tu kikamilifu kabisa.

Na wakati, kesho yake, akarudi, nikasema, “Naam, Bw. Wood?”

30 Akasema, “Vema,” kidogo aliongea kigeni, akasema, “mtu yeyote anaweza kuwaona samaki kabla ya kuwakamata, na kutaja ninii yao . . . kuwataja hadharani,” kasema, “Nadhani hilo ni sawa.” Na kwa hiyo sasa, ameokoka na kujazwa na Roho Mtakatifu.

31 Siku moja tulikuwa tumeketi, mimi, Lyle, na ndugu yake, tulikuwa huko chini tukivua samaki, miaka kadhaa iliyopita, ama mitatu. Naye mvulana wangu mdogo, kabla sijaondoka . . . Hatuwapendi paka nyumbani mwetu. Sasa, ikiwa unao, hiyo ni sawa, Siongei dhidi ya maskini paka wako sasa, lakini sipendi vitu hivyo, kwa hiyo, ama mbwa wa nyumbani, siwezi kuwavumilia. Kumpa upendo wa mtoto mchanga, huku unapanga uzazi, kisha kumpa maskini mbwa mwenye pua bapa upendo huo. Jamani! Mbona, ni—ni aibu. Hiyo ni kweli. Samahani usemi huo. Hiyo ni . . . sininii . . . Mnajua ninachozungumzia hata hivyo ninapolisema.

32 Kisha msichana wangu mdogo akaja na kusema, “Loo, Baba, jambo baya sana limetukia.” Kasema, “Mtu fulani alimtupa maskini paka mmoja,” yeye na msichana mwingine mdogo huko chini mtaani, kasema, “amekula sumu.” Kasema, “Maskini kitu hicho kitakufa, hivi huwezi—huwezi kumruhusu aingie kwa muda kidogo?”

33 Nikasema, “Yuko wapi huyo paka?” Nikaenda nikamchukua huyo paka, nikamwangalia, nikasema, “Nenda ukalete boksi,” na bila shaka, kesho yake asubuhi tulikuwa na watoto kadhaa wa paka.

34 Na kwa hiyo kesho yake . . . Kwa hivyo mvulana wangu mdogo, maskini . . . yeye ni mvulana kwelikweli, alikuwa amemshika mmoja mkononi namna *hii*, jamaa mdogo sana, kisha akamwangusha, ndipo maskini huyo jamaa akapinduka tena na tena. Nilichukia hilo sana, nilidhani amemwua, nikamlaza nyuma. Maskini paka mchanga, asingeweza kujizuia kuwa paka. Kwa hiyo basi, akaanza kubingirika.

35 Ndipo, tulikuwa tunaenda kuvua samaki usiku huo. Basi kesho yake nilikuwa nikivua samaki kijenye kwa chambo (Mnajua maskini samaki kijenye ni nini, maskini brimu, mnawaita hapa, nafikiri, kutia chambo katika ndoana.) huko chini kabisa Kentucky chini yetu, yapata maili mia moja na ishirini. Nami nilikuwa nimeketi pale, ndipo Roho Mtakatifu akakaribia, ndani kwenye mashua tulimokuwa, akasema, “Mtakuwa na ufufuo wa uhai moja kwa moja.”

36 Nikageuka na kumwambia Ndugu Banks jambo hilo, huku ameketi pale pale. Ikiwa kumewahi kuwa na mtu mzuri, mkweli, mwaminifu, huyo ni yeye na familia yake. Naye akasema, “Unafikiri itakuwa nini?”

37 Nikasema, “Huenda ikawa ni yule paka mdogo ambaye Joseph alimwangusha. Tutakapoenda nyumbani kesho, maskini paka huyo, labda . . . ” Mimi . . . Mlisikia hadithi ya yule oposamu, na kadhalika, ilikuwa katika *Wafanyabiashara*, na kadhalika. Kwa hiyo nikasema, “Pengine ni huyo.”

38 Usiku huo hatukukamata samaki hata mmoja. Kesho yake asubuhi tulikuwa . . . hatukuwa na samaki kabisa, kwa hiyo tukaingia kwenye ghuba dogo . . . kidogo baada ya mapambazuko, kuwakamata samakibrimu wakubwa, nami nilikuwa na ugwe wa kuvulia uliotupwa nje.

39 Ndugu yake, Lyle, alikuwa pamoja nasi, ndio kwanza aokoke majuma machache tu kabla ya hapo. Naye alikuwa na ndoana kubwa ndefu mno, naye akaweka mdudu juu yake, naye alikuwa na ugwe mkubwa wa kushusha, na kuushikilia chini namna *hii*, nguzo ya kupepesuka. Ndipo maskini samakibrimu mdogo akaumeza wote ukaingia tumboni mwake, badala ya kumnyakua tu upesi, kumvuta nje, ili aweze kumweka kama chambo, mbona, a—alimwacha aumeze mpaka chini.

40 Akasema, “Sasa, angalia pale vile kitu hicho kilivyofanya.” Naye akamshika tu yule samakibrimu kwa mkono mmoja, akazungushia ugwe kwa huo mwingine, na kuyavuta tu matumbo, mashavu, na kila kitu nje, akamrusha nje majini. Alikuwa tu maskini samakibrimu mdogo *hivyo*. Naye akafurukutika mara nne au tano, nayo maskini mapezi yake madogo yakatanuka, akafia majini, Na kwa hiyo, akamwangalia, akasema, “Jamaa mdogo, umepumua ya mwisho.” Huo ni usemi wa kale wa kusini. Ni wangapi waliopata kuusikia? Ninyi nyote wa kusini mliusikia, sivyo?

41 Kwa hiyo, naye alikuwa amelala pale, alielea pale karibu nusu saa. Nami nilikuwa . . . Nikasema, “Lyle, una ndoano kubwa kupita kiasi, Ndugu.” Nikasema, “Ingiza tu ndoano yako na maskini namba kumi na mbili, kama unaweza kuipata hapo. Basi mara tu yule samaki . . . ” kuwaonyesha jinsi ya kuwavuta hao samakibrimu wadogo.

Akasema, “Loo, mimi ni mvulana mshamba tu.” Kasema, “Hivi ndivyo unavyolifanya,” namna hiyo.

42 Nami nikaketi pale yapata nusu saa, ndipo maskini yule samaki akafa, akaelea humo majini, naye akaelea tena ndani ya baadhi ya yungiyungi, moja kwa moja kwenye kitu kama ghuba ndogo.

43 Nilikuwa nimeketi pale, kwa ghafla . . . Ni katika milima ambapo Mto Wolf umezuiliwa, nao wakafanya bwa—bwawa kwa ajili ya kiwanda cha nguvu za maji. Na ni . . . Nadhani kuna maili mia moja na hamsini za maji, ndani na nje tu ya milima hii. Naye Roho wa Bwana, kama sauti kuu ya upepo, akashuka kupitia hapo kwa kasi, akaingia ndani ya hiyo mashua, akasema,

"Simama." Kasema, "Nena na maskini huyo samaki, atapokea uhai wake."

44 Hapo alilala maskini samaki huyo, amelala hapo amekufa juu ya maji kwa muda wa nusu saa, nikasema, "Ewe samaki mdogo, Yesu Kristo anakupa uhai wako. Katika Jina la Yesu Kristo, ndivyo ilivyo." Na mara niliposema hivyo, maskini huyo samaki akageuka namna *hiyo*, akaenda *rrruut*, akaogelea majini. Sasa, hii hapa Biblia mbele yangu, Mungu ndiye Hakimu wangu, Ndugu Banks ni shahidi.

Lyle nusura tu azimie, ndani ya mashua, akasema, "Hiyo ilimaanisha mimi, kwa sababu nilimwambia yule samaki mdogo 'Umepumua ya mwisho.'"

Nami nikasema, "La."

45 Ndugu Banks alisisimkwa, akasema, "Ninajisikia kama Petro: 'Hebu tujenge vibanda vitatu na tukae hapa.'" Akasema, "Hili ni zuri." Ndipo akaanza kuelezea kwamba ni watu wangapi ulimwenguni kote wangetaka kuwa wakiketi pale, na wangeona hilo. Kisha kasema, "Wazia juu yetu sisi," kasema, "Mashahidi wa Yehova, halafu Mungu anatuvuta kando akatuleta hapa, na kuona mambo haya yote ambayo tumeona juma hili. Na jambo hili hapa linatukia, kulisikia likitabiriwa jana, hili hapa linatukia leo," na namna hiyo.

46 Nikasema, "La, haikuwa hivyo. Hiyo ni kuonyesha tu neema Yake." Nikasema, "Angalieni, kwenye orodha yangu nyumbani nina takriban watoto thelathini au arobaini wenye kifafa, nikiwaombea." Kisha nikasema, "Nina, sijui ni wagonjwa wangapi wa kansa, wanaokufa. Kuna watu wamelala mahotelini, nasubiri kuona Bwana atasema nini. Naye Huyu hapa anakuja na kuniambia kuhusu samaki mdogo."

47 Mnaona, inaonyesha Yeye angali ni Mungu. Kulikuwa na maelfu ya wenye ukoma waliokuwa wamelala katika siku za Bwana Yesu, kulikuwa na vilema, viwete, waliopindika, vipofu, na wanaoteseka, na hata hivyo Mungu alitumia nguvu Zake kuulaani mti. Mti ulinyauka kwa Sauti ya Bwana Yesu, ili tu kuwaonyesha ya kwamba—ya kwamba Yeye anajali miti Yake, samaki Wake, anajali kila kitu; inaonyesha kwamba Yeye anajua kila kitu, Naye hufanya kila kitu vema. Mambo mengi sana yangeweza kusemwa.

48 Ninawaona baadhi ya rafiki yangu, ninamwona Bibi Ungren ameketi pale, sikujua ulikuwa mkutanoni, na nimejua leo ya kwamba Ndugu Myers na Dada Myers, walikuwa hapa. Wako wapi? Mimi . . . Unajua, Ndugu Myers, umekuwa mdogo zaidi, sikukujua, Dada Myers. Watu hao wametoka mbali sana huko Nashville, Tennessee, hapa juu mkutanoni.

49 Sikujua hadi leo kuwa mlikuwa mkutanoni, nimejua leo. Mmekuwako wakati wote? Vema, sijaninii . . . Sikujua hilo. Nilifikiri mama mkwe wako na shemeji yako walikuwa

wamerudi nyumbani kutoka kwenye mkutano mwingine, na hapa ninawaona usiku wa leo, nikaangalia pale, nikasema, "Yuko hapa mahali fulani." Kwa hiyo, ningeweza kumwona.

50 Maskini Nashville, ni mji mashuhuri, umeshikilia shuhuda nyingi nzuri. Je, nina wakati kwa ajili ya mmoja zaidi kutoka Nashville? [Ndugu mmoja anasema, "Hakika."—Mh.] Ni sawa? Samahani. Nilikuwa nimetoka Dallas. Jambo hili moja linahusu Nashville, kwangu mimi, na hilo lilikuwa, jambo moja, nilimwita mhubiri kutoka Nashville, wakati mmoja huko Jonesboro, aliyeishi moja kwa moja nje ya Nashville kule, kwa namna fulani nimekuwa nikiiruka tangu wakati huo. Wengi wenu ninyi ndugu wa Mwungano wa Kipentekoste mnamjua vizuri sana, ndugu mzuri. Lakini alikuwa ameketi pale huku haamini, nami nikaliita jina lake. Mnaona? Na . . . [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . . sijawahi kumwona maishani mwangu. [Sehemu tupu kwenye kanda.] . . . mambo na . . . [Sehemu tupu kwenye kanda.] . . . vibaya kweli. Na kwa hiyo ni—nikalisimamisha basi. Ilikuwa kwa Ndugu Reed huko Jonesboro, ambapo mtu huyo alifichuliwa.

51 Lakini nakumbuka usiku mmoja nilikuwa nikitoka Memphis, nikiruka kwa ndege nikija nyumbani, nao wakakumbwa na dhoruba, ndipo wakanishusha huko Memphis, imekuwa miaka mingi iliyopita. Nao Memphis uko kwenye Mto Mississippi, kama sote tujuavyo. Na kwa hiyo wakanipeleka kwenye hoteli hiyo maarufu, Hoteli ya Peabody, nami nikawazia, "Jamani, wakati mmoja nitakuwa kabaila, nikikaa kwenye hoteli hiyo."

52 Kwa hiyo wakanipigia simu baada ya muda kidogo na kusema, "Vema, kila kitu kitakuwa sawa," mwendo wa saa nne hivi. Kasema, "Jiweke tayari, tutaninii . . . Ndege inaondoka asubuhi saa moja."

"Asante, Bwana."

Kasema, "Jiweke tayari, limosini, itakuchukua."

"Sawa, Bwana."

53 Wengine wengi walikuwa humo hotelini usiku huo. Kwa hiyo nikakaa hadi saa sita, nikiwaandikia watu mbalimbali barua, na kuomba na . . . juu ya haja nilizokuwa nazo, nikijibu barua fulani ya kibinafsi ambayo ilikuwa imewekwa kwenye mifuko yangu kote mkutanoni.

54 Kesho yake asubuhi nikaamka mapema, nami nikawaza, "Vema, thenashara ninaamini nitatoka na kutafuta sanduku la posta, na kuzituma," mwajua, niziweke humo ndani.

55 Kwa hivyo basi, nikaenda kwenye sanduku hili, nami nikafikiri ningelipata. Nikashuka barabarani, nikaanza kutembea barabarani, ndipo niliposhuka barabarani kidogo, nikaanza kuvuka barabara ambapo palikuwa na askari mkubwa

Mwairishi amesimama pale nje, naye angepiga filimbi, nao watu wangevuka. Ndipo Kitu fulani kikaniambia, “Rudi upitie hiyo njia nyingine.”

56 Je, mnaamini watoto wa Mungu wanaongozwa na Roho wa Mungu? Ninataka tu kuwasikia mkisema hivyo, ili niweze kuimaliza hii hadithi. Hiyo ni kweli. Naye hufanya kazi kwenye miisho yote miwili ya mstari, mnaona, daima huzifanya pembe Zake kukutana. Nami nikawaza, “Vema, labda Huyo alikuwa ni mimi tu nikiwazia hilo,” lakini ilisikika kama Sauti fulani iliniambia.

57 Kulikuwa na duka la bidhaa za michezo pale, na jinsi ninavyopenda uvuvi na uwindaji, nikaenda tu kwenye dirisha la hilo duka la bidhaa za michezo, nami nilikuwa nikiangalia pande zote pale nione kwamba sikuvutia usikivu wa askari huyu mkubwa, labda angenifukuza pembeni. Nami nikasimama hapa na nikatazama huku na huku, hakuna mtu aliyekuwa akiniangalia, kasema, “Baba wa Mbinguni, huyo alikuwa ni Wewe? Sitaki kukukosa, Baba. Je, huyo alikuwa ni Wewe?”

Ndipo Sauti dhahiri tu kama vile unavyonisikia, ikasema, “Geuka urudi.”

58 Vema, nikageuka na kuanza kurudi nyuma, nami nikatembea na kutembea, mpaka nikafika upande wa pili na kushuka kwenye maeneo ya watu weusi, huko chini kabisa kuelekea mtoni. Nikashuka kwa njia hiyo, nayo ilikuwa ni asubuhi nzuri, nikaangalia juu, nilikuwa nimeenda, basi, zaidi ya saa moja, nikawazia, “Mbona, ndege imeondoka!”

59 Lakini kitu Fulani kikaendelea kusema, “Endelea kutembea.” Nami namjua Mungu vizuri vya kutosha, endelea tu kufanya kile anachokwambia, fanya. Usiwe, usitumie mawazo yako mwenyewe, fanya kile anachokwambia, fanya, endelea tu. Nikaendelea tu kutembea, kutembea, nikashuka ambako wanakaa watu weusi, maskini nyumba ndogo huko chini, ndipo nikaangalia . . . Nilikuwa naenda huku nikiimba ule wimbo mdogo ambao ninyi Wapentekoste mlikuwa mkiuimba kila wakati. Hebu tuone, mimi—mimi huuimba mara moja moja, najaribu kuukumbuka, kitu kuhusu:

Walikuwa wamekusanyika katika chumba cha juu,
Wote wakiomba katika Jina Lake,
Walibatizwa na Roho Mtakatifu,
Ndipo nguvu za utumishi zikaja; (Mmewahi kuusikia huo?)
Aliyowafanyia siku hiyo
Atakufanyia yayo hayo,
Furaha kuwa naweza kusema mimi ni mmoja wao.

Nilikuwa ndio kwanza nijifunze huo, na nilikuwa nikishuka nikisema:

> Mmoja wao, mmoja wao, (*Bwana, unataka nifanye nini?* Mnaona?)
> Nina furaha sana kwamba ninaweza kusema mimi ni mmoja wao.

60 Naye Roho Mtakatifu anaendelea tu kusema, "Endelea mbele, endelea." Unajua jinsi unavyoongozwa na Roho. Nikaendelea tu kushuka barabarani nikiimba, mwajua, na kuimba.

61 Baada ya kitambo kidogo nikaangalia, akiegemea kwenye maskini ua uliopakwa chokaa, kibanda kidogo nyuma yake, alikuwa ni maskini Shangazi Jemima wa kawaida amesimama huku amejizungushia shati la mwanamume kichwani mwake, mashavu manene mno, nikaacha tu kuimba, ilikuwa yapata umbali wa huu mlango, nikaanza tu kutembea barabarani.

Nilipopita hapo, akasema, "Habari za asubuhi, Kasisi."

Vema, nikawazia, "Ngoja kidogo." Sasa, ati *kasisi*, hilo linamaanisha "mhubiri" huko kusini. Mnaona?

"Habari za asubuhi, Kasisi."

62 Nami nikageuka, nikasema, "Habari za asubuhi, Shangazi." Kwa kawaida hivyo ndivyo tunavyowachukulia watu weusi huko chini, "Habari za asubuhi, Shangazi." Nilikuwa . . . Alikuwa akicheka, machozi makubwa mno yakitiririka kutoka kwenye mashavu yake makubwa meusi, alionekana kama Malaika kwangu, amesimama pale akitazama, akasema . . .

Nikasema, "Aisee, jambo lingine, ulijuaje kuwa mimi ni kasisi?"

Akasema, "Nilijua ulikuwa," kasema, "kitu pekee, ulipaswa kuwa na mkoba mkononi mwako."

Nikasema, "Niliuacha *kule* juu, na kuziweka tu barua chini ya mkono wangu." nikawazia, "Aa-ah!" Nikasimama.

Naye akasema, "Nilijua ulikuwa unakuja." Kasema, "Ulikuwa na kofia hiyo kando ya kichwa chako, na kidogo ni ya kijivu, umevaa suti hiyo ya kijivu."

Nikasema, "Naam, Mama."

Akasema, "Je, umewahi kusoma ile hadithi katika Biblia kuhusu yule mwanamke Mshunami?"

Nikasema, "Naam, Mama, nimeisoma." Nikaukaribia huo ua.

63 Akasema, "Nilikuwa mwanamke wa aina hiyo. Sikuwa na watoto, bali mimi ni mwanamke mfua nguo, lakini mimi na mume wangu ni Wakristo." Kisha akasema, "Ni—niliomba kwa miaka miwili ili Bwana anipe mtoto." Pia kasema, "Nilimwahidi Bwana kama angenipa mtoto, nitamlea kwa heshima Yake." Basi

akasema, “Siku moja mvulana mdogo mzuri alizaliwa nyumbani kwetu.”

64 Akasema, “Kasisi, nilimlea kadri nilivyojua apate kumtumikia Bwana, lakini alitoka akaingia miongoni mwa watu wabaya, ndipo akashikwa na ugonjwa wa zinaa,” kaswende, kisha kasema, “wala sisi hatukujua, tukiwa familia ya Kikristo, hatukujua hilo.” Halafu kasema, “Kamwe hatukuninii . . . Wala yeye hakuwazia chochote juu yake” kisha kasema, “ukaingia moyoni mwake.” Tena kasema, “Mtu-daktari anasema kwamba hawezi kuishi,” na kasema, “sehemu fulani za moyo wake zimeangamia.” Ndipo kasema, “Tunamdunga sindano za kila namna. Naye sasa amepoteza fahamu, hii ni siku ya tatu.” Naye akasema, “Kasisi, amelala *mle* ndani akifa.” Kisha kasema, “Hajajua lolote sasa, hii ni siku ya tatu.”

65 Kisha kasema, “Jana usiku niliomba usiku kucha.” Akasema, “Niliomba, ‘Bwana, umenipa mtoto huyu kama vile ulivyompa yule mwanamke Mshunami, lakini yuko wapi Elisha Wako?” Basi akasema, “Nikalala, kisha nikaota ndoto kwamba niliona mtu akija, naye alikuwa amevaa kofia ndogo ya kijivu, na suti ya kijivu.” Naye akasema, “Nimesimama kwenye lango hili tangu kabla ya mapambazuko asubuhi ya leo, nikikungojea ushuke kuja barabarani.”

66 Mungu hujibu kwenye miisho yote miwili ya mstari. Nikamtazama, nikampiga-piga mgongoni. Alikuwa na unyevunyevu kutokana na kusimama hapo. Nikamtazama kidogo, naye akasema, “Je, waweza kuingia ndani?” Ndipo nikaingia, lango kuukuu lenye ncha ya jembe likining’inia juu yake kama uzito wa kulivuta pamoja.

67 Alipofungua m—mlango wa hicho kibanda kidogo cha kale, kibanda kidogo tu cha kawaida chenye kitanda kidogo cha safari cha chuma (Ni wangapi wanaojua hicho ni nini, maskini kitanda kidogo cha chuma?), wala hakukuwa na zulia sakafuni, kusini haswa, lakini alikuwa na bango lililoning’inia mlangoni, “Mungu ibariki nyumba yetu.”

68 Nimekuwa kwenye ikulu za wafalme, nilimwombea Mfalme George wa Uingereza, mwajua, alipoponywa kukacha kwa seli, niliwaombea wafalme wengine, watawala wakuu, wafalme, nimekuwa katika baadhi ya nyumba bora zaidi Marekani, lakini sikuwahi kujisikia kukaribishwa zaidi ya vile nilivyojisikia pale pale, maskini makazi hayo ya watu weusi asubuhi hiyo.

69 Nikatazama, amelala pale kitandani, palikuwa na mvulana mkubwa mno, mzuri, alionekana kuwa na uzito wa takriban ratili mia moja na sabini au themanini, urefu wa futi sita. Naye alikuwa na blanketi, dogo, kama shuka dogo la blanketi mkononi mwake, naye alikuwa akifanya, “Uuum, uuum!” Akaendelea kulalamika juu ya kuwa na “giza,” akasema, “giza humu ndani.”

Nikasema, “Anazungumza.”

70 Akasema, “Amekuwa akisema hivyo kwa siku mbili.” Kasema, “Anafikiri yuko huko nje baharini mahali fulani, naye amepotea kwenye mashua, wala hawezi kupata njia yake ya kurudi.” Akasema, “Kasisi, moyo wangu wote, kama ninaweza tu kumsikia akisema ameokoka, anaweza kuondoka basi.”

Nikasema, “Shangazi,” nikasema, “jina langu ni Branham, ninawaombea wagonjwa. Je, umewahi kusikia kuhusu huduma yangu?”

Akasema, “La, bwana, Kasisi Branham, sijapata kusikia habari zako.” Akasema, “Samahani.”

Nikasema, “Je, unaamini Mungu anaweza kumponya mvulana huyo?”

Hilo hata halikumvutia, alitaka aokoke. Alitaka ili aweze kukutana naye Huko.

71 Nami nikasema, “Sawa, na tuombe.” Basi tukapiga magoti kando ya kitanda, nikaigusa miguu yake. Sasa, ilikuwa baridi, inanata, sijui, mnaona. Basi nikapiga magoti kando ya kitanda kuomba, na nikasema, “Shangazi, vipi wewe ukiomba kwanza?”

72 Nimesikia maombi mengi sana, nawaambia wakati maskini mtakatifu huyo alipoanza kuzungumza na Mungu, ulijua alikuwa amezungumza Naye hapo awali. Maombi ambayo alisema kwa huyo...kwa Mungu asubuhi hiyo, alisema, “Bwana, unajua sikuzote nimekuheshimu, nimekupenda, nimefanya kazi, nimekufanyia haya yote, si kwamba ninastahili, Bwana, lakini laiti ningalimsikia tu mvulana wangu akisema ameokoka!” Akasimama.

73 Sikusema lolote, nilimwangalia tu, kamwe sikuomba, nilimwangalia tu. Akasimama, akavuta blanketi juu yake tena, alikuwa tu amevaa kitu kama kijisuruali cha kipande, ndipo akambusu kwenye paji la uso na kusema, “Mungu ambariki mtoto wa Mama.”

74 Nilisimama tu pale, nimepiga magoti, hasa, chini ya kitanda, nikitazama, nikiishika miguu yake, nami nikawazia, “Hiyo ni kweli. Haidhuru ameleta fedheha kiasi gani, ni mkubwa jinsi gani, ama chochote kile, amelemewa kiasi gani na ugonjwa wa zinaa, na kile ameifanyia hiyo familia, mama hawezi kumsahau mtoto wake.”

75 Ndipo nikawaza, “Ikiwa mama hawezi kumsahau mtoto wake anayenyonya! Yesu alisema, ‘Siwezi kukusahau, kwa sababu jina lako limechorwa katika vitanga vya mikono Yangu.’ Jinsi upendo wa Mungu! Haidhuru tumefanya nini huko...” Nilitazama jambo hilo, nusura moyo wangu uvunjike. Nami nikasema, “Sasa, tutaomba, Shangazi, nitaomba pia.”

76 Akasema, “Asante, Kasisi,” naye akapiga magoti tena, akakunja mikono yake, naye akainamisha kichwa chake chini

juu ya huyo mvulana, nikashika miguu yake. Akaendelea kufanya "Uuum! Kuna giza, huku kuna giza."

77 Nami nikasema, "Baba wa Mbinguni, sasa nimechelewa kwa saa mbili kutoka kwa ndege yangu, lakini nilitii Neno Lako tu. Hakika hapa ndipo mahali pale, sijui ni wapi kwingine, ndipo mahali pekee nilipopapata. Wala sijui lolote kuhusu mvulana huyu na kuhusu mwanamke huyu, bali Wewe ulinionguza hapa kwa njia ya ajabu. Naye alisema amekuwa akiomba, naye aliniona katika ndoto asubuhi ya leo, nikimjia. Kwa hiyo jambo pekee nijualo kufanya ni kusimama na kumwombea maskini mvulana huyu. Havutiwi na uponyaji wake, lakini anataka aokoke. Ninaomba, Mungu . . . "

78 Yapata wakati huo, akasema, "A-ha, Mama. Nuru inaingia humu chumbani." Dakika chache alikuwa ameketi kando ya kitanda, akiongea nasi.

79 Nikaondoka, nikasimamisha teksi, nami nilikuwa nimechelewa kama saa tatu kwa ndege yangu wakati huo, ni, loo, labda zaidi ya hizo, ilikuwa yapata saa tatu na nusu. Nikamwambia dereva, nikasema, "Nipeleke kwenye uwanja wa ndege." Nilikuwa nimeacha kila kitu, nikapitia pale na kuchukua mkoba wangu na kadhalika, nikaendelea mbele. Na mara nilipokuwa nikiingia langoni, kasema, "Wito wa mwisho kwa safari 23 ya ndege kuelekea Louisville, Kentucky."

80 Jambo ni kwamba, wazieni, imani rahisi ya huyo, samahani, rafiki yangu mweusi, imani rahisi ya mwanamke huyo mweusi asiye na elimu iliishusha ndege hiyo, na kuishikilia pale.

81 Yapata miaka miwili baadaye nilikuwa nikienda Phoenix. Nilisafiri kwa gari-moshi, nanyi mwajua, kwenye gari-moshi inakubidi kutumia pesa nyingi sana kwa maskini sambusa hizo, huku zimekatwa vipande vinene sana inaninii tu . . . nyembamba sana hivi, zina upande mmoja tu, na takriban senti hamsini kwa sambusa. Sikuweza kustahimili hilo, ghali sana kwangu.

82 Kwa hivyo tukaingia Memphis, ikiwa unajua, unaingia kutoka mashariki kwenda magharibi. Gari-moshi likasimama hapo ili kuwasha jukwaa-mzunguko. Basi liliposimama, kulikuwa na kituo kidogo cha hambaga pale, nami nikaruka nikaanza kukimbia kupitia pale nikanunue kifurushi kizima cha hambaga, za kutosha kunifikisha Phoenix. Unazipata kwa kama senti kumi kila moja pale, hiyo ilikuwa ni bora kuliko kwenye gari-moshi.

Kwa hivyo nikakimbia kujinunulia kifurushi cha hambaga, ndipo nikamsikia mtu akisema, "Aloo hapo, Kasisi Branham!"

Nikatazama pale, pale palikuwa na kofia nyekundu amesimama pale, nikasema, "Aloo, Mwanangu," nikaanza kushuka chini.

Kasema, "Kwani hunitambui?"

83 Nikaangalia nyuma, nami nikafikiri labda nilimfahamu wakati mmoja ama chochote kile, nikawaza, "Hapana, sijawahi kuwa huku." Nikasema, "Hapana, siamini nakujua."

84 Kasema, "Unakumbuka kama miaka miwili iliyopita, ulikuwa huku chini?" Kisha kasema, "Ulikuja huku, nyumbani kwangu asubuhi moja, naye Bwana akakuongoza kule, ndipo ukaniombea nami nilikuwa nimelala mahututi?"

Nikasema, "Wewe siye yule mvulana!"

Akasema, "Naam, ndiye mimi." Akasema, "Mimi—mimi—mimi—mimi—mimi—mimi nimeponywa, na nimeokoka sasa, Kasisi Branham." Loo, jamani! "Nimeokoka sasa, Kasisi Branham."

85 "Neema ya ajabu, jinsi inavyosikika tamu!" Jinsi ningeweza kusimama hapa kwa saa nyingi! Nimeanza kuzeeka sasa. Nina miaka thelathini na mmoja katika huduma, nikisafiri kote ulimwenguni, tamasha na kadhalika, kuchukua tu mikutano na kushuhudia, lakini, loo, vema.

86 Tutakapofika—tutakapovuka ng'ambo ya pili, nataka miadi na kila mmoja wenu, ninataka kuketi chini kwa miaka elfu moja na kila mmoja wenu. Hatutakuwa na wakati pungufu wakati sote tutakapomaliza kuliko tuliokuwa nao tulipoanza, mnaona. Kuketi chini tu na kuzungumza juu ya kila jambo. Si itakuwa ni ajabu tutakapokutana huko? Bwana awabariki.

87 Sasa, marafiki, sisi si wasafiri na wageni pamoja nanyi nyote, sisi ni wasafiri na wageni kwa ulimwengu.

88 Sasa, kuna baadhi ya watu hapa ambao ni wageni kutoka nje ya mji. Sasa, kesho ni Jumapili, sitawaweka muda mrefu sana, usiku wa leo. Sijali mkikosa kazi ya siku moja, lakini kamwe msikose shule ya Jumapili, kwa lolote mfanyalo. Lazima mhudhurie shule ya Jumapili.

89 Sasa, kuna makanisa mazuri hapa. Hili ni mojawapo, nao wachungaji hawa nyuma hapa ni watu walio na makanisa ambayo yanafadhili mkutano huu. Wanawakilisha Injili hii, wanasimama hapa. Wao . . . Kama hawakufanya hivyo, wangekuwa nje ya jukwaa. Hiyo ni kweli. Nao wamesimama hapa kama watu wa Mungu wanaoamini na wanafadhili mkutano huu. Wana makanisa hapa, labda ya kanisa lenu la kimadhehebu, nao wako—wako hapa. Wangefurahi kuwa nanyi, nami nina hakika wangewafanyia mema, kwenda kuwasikiliza kesho. Ningefanya hivyo kesho asubuhi kwa ajili ya shule ya Jumapili.

90 Na kesho alasiri ibada zitarudi hapa maskanini, ama, kanisani. Samahani, naendelea kusema "maskani." Ninii . . . Vema, maskani ni mahali pa kukutania. Hiyo ni kweli. Kwa hiyo inawakilisha hema la kukutania jangwani. Na kwa hiyo—kwa hiyo sisi—tunatarajia kuwaona hapa kesho alasiri. Saa ngapi?

Saa nane, ama kitu kama hicho, saa nane ama saa nane na nusu kesho alasiri. Sasa, hakikisheni kuhudhuria shule ya Jumapili.

91 Nami nataka kuwaambia jambo fulani: Ni dhambi kuwatuma watoto wenu kwenye shule ya Jumapili. Mnajua hilo. Ni dhambi kuwatuma, inawapasa kuwapeleka. Daima wapelekeni, mnaona. Ninyi nendeni pia.

92 Niliona katuni ndogo gazetini si muda mrefu uliopita: Marekani Mamboleo. Hao hapo mama na baba wamelala pale, na huku chupa za pombe na makopo yametapakaa sakafuni, na sigara zinatoa moshi sakafuni, na mambo kama hayo. Yapata saa tatu, mvulana mdogo tayari amesimama, amenawa uso wake, na kuvaa nguo, anabisha mlangoni, kasema, "Nani atanipeleka shule ya Jumapili?" Hiyo ni kweli. Hivyo ndivyo ilivyo. Mungu aturehemu.

93 Marafiki, mimi ni. . .Mnaweza kufikiri mimi ni katili, lakini sikusudii kuwa hivyo. Mimi. . .Dhambi hunikera sana. Ninapoona, ikinyemelea Kanisani mwangu, loo, jamani, ninalionea wivu Kanisa hili. Na—nalionea. Hiyo ni kweli. Mungu aliniitia Kanisa hili. Na—naweza. . .Mnafikiri ninawaudhi, natumaini siwaudhi, natumaini mnaelewa. Natumaini Roho Mtakatifu atawajulisha tu, katika to—toni ya sauti ninayotaka, awajulishie. Mnaona? Aminini tu. Mungu awabariki. Hebu tuzungumze na Mwandishi sasa kabla ya kulifungua Neno.

94 Baba yetu wa Mbinguni, tusaidie usiku wa leo, sasa. Shuhuda hizi, jinsi tungeweza tu kusimama, na tutakapofika pale na kumwona Danieli, na loo, nataka kusimama kwa miaka elfu moja na kumsikiliza tu! Ninataka kuwaona Mathayo, Marko, Luka, Yohana, Paulo, Barnaba, loo, nataka kuwaona wote, lakini zaidi ya yote, nataka kumwona Yesu.

95 Nasi tutakaposimama kule, wakati Malaika wanapopiga kambi kuizunguka dunia hii huku vichwa vimeinamishwa na kutusikia tukiimba nyimbo za ukombozi, hawajui tunalozungumzia, hawakupotea kamwe, haikuwabidi kukombolewa. Lakini tutakapomvika taji Mfalme wa mfalme, na Bwana wa bwana, na kuimba nyimbo za Sayuni, "Kukombolewa kwa Damu ya Mwana-Kondoo," itakuwa ni wakati wa jinsi gani! Tunaitazamia saa hiyo.

96 Utubariki usiku wa leo. Tunakuja kufanya ushirika kwenye Neno Lako, Bwana. Tusaidie sasa, na ulitie Neno mafuta. Jalia litoke liende kama Upanga, na kutahiri ulimwengu wote mbali nasi. Maana tunajua watoto wa Mungu wametahiriwa mioyo na masikio na Roho Mtakatifu. Tunaomba ya kwamba atautahiri moyo na masikio yangu, usiku wa leo, atahiri kila moyo na sikio hapa, usiku wa leo, ili kwamba, katika kusikia, tuweze kusikia; katika kuona, tuone; katika ufahamu, tutambue, na tuokolewe na kuponywa kwa ajili ya Ufalme wa Mungu. Tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

97 [Ndugu mmoja anasema, "Ndugu Branham, kuna simu ya dharura. Naweza kutangaza hilo?—Mh.] Naam. ["Simu ya dharura ya Mchungaji Wall, anaombwa arudi ofisini, tafadhali."]

98 Kama ni ugonjwa, itangaze jukwaani, Mchungaji, tutangazie hapa, tutaomba mara moja. Wakati amekwenda . . . Hatujui . . . Ni dharura, lazima iwe ni kitu fulani . . . [Ndugu huyo anasema, "Huyu ni mtu anayekufa, katika kanisa lake, ambaye anamwita. Tunaweza kumwombea."—Mh.]

Loo, naam, mtu mgonjwa sana, katika hali ya kufa, katika kanisa lake. Mchungaji Wall, Mungu ambariki. Hebu tuinamishe vichwa vyetu.

99 Baba yetu wa Mbinguni, mchungaji huyu mwenye neema sasa, akienda kwenye simu kusikia mmoja wa kusanyiko lake akiita. Baba wa Mbinguni, bila shaka mchungaji huyo sasa anakumbuka hizo saa na miito ya madhabahuni, na mambo ambayo amefanya, akitumaini sasa ya kwamba kila kitu kiko sawa. Sio jambo baya, tunapokuwa tayari kwenda, Bwana, ni ajabu, "Ina thamani machoni pa Bwana mauti ya watakatifu Wake."

100 Sasa, Baba, ikiwezekana, mwachilie, sivyo, Bwana, kwa ajili ya ibada usiku wa leo? Acha iwe wakati mwingine, kama wakati wa huyo mtu umeitwa, jalia aishi muda kidogo zaidi, Bwana, katika jibu la maombi tu. Tujalie, Baba.

101 Ifariji mioyo ya wale wanaomtazamia. Jalia tukumbuke, Bwana, kwamba miili yetu ni dhaifu, sisi ni mavumbi, mavumbini tunarudi. Lakini jalia tumkumbuke Muumba wetu sasa huku tukiwa na akili timamu na tunaweza kuja madhabahuni kwa akili timamu na kwa busara na kumpokea Kristo kama Mwokozi wetu. Mbariki Ndugu Wall, Bwana. Ninamwombea, nami ninamwombea yule anayekufa. Katika Jina la Yesu. Amina.

102 Nina Maandiko na muktadha hapa ambao ningependa kuzungumzia kwa dakika chache tu. Je, mnaweza kunisikia vizuri kutoka hapa? Hilo ni sawa. Nataka mfungue pamoja nami kwa usomaji wa Maandiko sasa.

103 Nami ninataka kutangaza, pia, kwa ajili ya . . . ibada kubwa ya uponyaji kesho tena. Je, mnge—mngependa ibada nyingine ya uponyaji kesho? Ni wangapi wangependelea? Tunataka kufanya yale tu ambayo Bwana angetutaka tufanye sasa. Na katika kusanyiko . . . Ni wangapi juu kwenye roshani wanafikiri tunapaswa kuwa na ibada kuu ya uponyaji kesho, kuwaombea wagonjwa? Hatujui kuhusu uponyaji, huo ni wa Mungu.

104 Vema. Nitamtuma Billy kuja kusambaza kadi za maombi alasiri, kabla tu ya . . . Mnasema, ni saa nane na nusu inaanza? Vema, atakuwa hapa saa saba na nusu basi, ama saa nane kasorobo, ama kitu kama hicho, ili aweze kuzisambaza hizo kadi kabla hatujawaombea wagonjwa. Vema.

105 Sasa, katika Wakorintho wa Kwanza, mlango wa 14, kifungu cha 8, ningependa kusoma jambo hili kwa ajili ya muktadha:

Kwa maana baragumu ikitoa *sauti isiyojulikana,* je, tunapaswa *kujiweka tayari* kwa *vita?*

106 Nitahubiri juu ya somo hilo, ama, kuzungumza kwa dakika chache juu ya somo la *Sauti Isiyojulikana.*

107 Sasa, tunaishi katika siku ya kutokuwa na uhakika. Ni wakati usio na uhakika. Nami ninataka kuwaulizeni jambo fulani. Na wakati tukininii . . . Ninajaribu kufundisha, kwa muda kidogo tu, na kurejea kwenye miktadha hii ambayo . . . hapa, na Maandiko, ningependa kuwaulizeni . . . Kitu chochote kisicho hakika hakiwezi kuaminika. Ikiwa hakina hakika, huwezi kukiamini. Paulo alisema hapa, "Baragumu ikitoa sauti isiyojulikana, tutajifanyaje tayari kwa vita?"

108 Sasa, kutokuwa na uhakika. Hakujapata kuwa na wakati ambapo mambo hayakuwa hakika kama leo hii. Na chochote kisicho hakika hakiwezi kuaminiwa. Kumbukeni hilo tu. Kitu chochote kisicho hakika hakiwezi kuaminiwa. Ikiwa kuna swali, usikifanye kabisa.

109 Mama fulani alinijia, muda si mrefu uliopita, mwanamke kutoka katika kanisa langu, msichana mdogo. Naye akaniambia . . . Wana aina fulani ya mtindo wa wasichana kuvaa sketi za kashfa, ama kitu kilichoonyesha hicho kipande kidogo, kilichokatwa *hivi*, kinachovaliwa na . . . kilionyesha sketi yao ya ndani. Naye akasema, "Ndugu Branham, unafikiri ni kosa kwetu sisi wasichana Wakristo kuvaa sketi za kashfa?"

Nikasema, "Kwa nini kuniuliza hilo?"

Akasema, "Nilikuwa tu nikishangaa."

110 Nikasema, "Ikiwa ni swali akilini mwako, usilifanye." Nikasema, "Ikiwa ni swali, achana nalo, huwezi kuwa na hakika. Vaa jinsi unavyojua kuwa una uhakika." Unaona? "Usibahatishe hata kidogo."

111 Nami nikasema, "Jambo lingine, kwa nini . . . " Nikasema, "Ni nini—ni nini sketi ya kashfa?" Sikujua alichokuwa akizungumzia, naye akaniambia ni nini, ndipo nikasema, "Msichana Mkristo angetaka kuonyesha sketi yake ya ndani kwa sababu gani jamani? Siwezi kuelewa." Mnaona, mnaona? Hiyo ni kweli. Kamwe si—siwezi kuona hilo akilini mwangu. Halina maana kwangu. Kristo ndiye Uzima wetu. Vema.

Sasa, lakini ikiwa kuna swali . . . Wanaume waje, waseme, "Je, unafikiri ni kosa kuvuta sigara?"

112 "Kwa nini kuuliza hilo? Likiwa ni swali niani mwako, achana nalo." Kwa kuwa chochote usichofanya kwa imani ni dhambi. Kweli. Inabidi iwe ni kwa imani. Basi unawezaje kuvuta sigara na kuwa na imani? Unaona? Ni . . . Moja kwa moja katika dhamiri yako mwenyewe, inakuonyesha kwamba umekosea.

Kwa hivyo ikiwa si la hakika, afadhali uachane nalo, maana hilo linaweza kuwa ndilo jambo moja linalokuweka nje ya Ufalme wa Mungu.

"Loo," unasema, "Ndugu Branham, jambo moja dogo kama hilo?"

Kitu kimoja kidogo kama hicho kitalisababisha, kutotii tu amri moja ya Mungu. Uasi mmoja mdogo, amri moja, ulisababisha magonjwa yote.

113 Pia angalieni, Yesu alisema katika Somo Lake Mwenyewe katika Mahubiri Yake, "Mkumbukeni mke wa Lutu." Sasa, alikuwa na udhuru mwingi zaidi kuliko tulio nao leo, tukifanya mambo tunayofanya. Watoto wa mwanamke huyo na wajukuu walikuwa wakiteketea katika Moto wa kuzimu uliotumwa kutoka kwa Mungu. Naye maskini huyo jamaa, akipiga mayowe na kulia akipanda kule, na akageuka tu kuangalia nyuma, ndipo akageuka kuwa nguzo ya chumvi, na anasimama pale hata wa leo, naye Yesu alisema, "Mkumbukeni mke wa Lutu." Hatuna budi kushika kila Neno la Mungu. Mnaona? Kitu kimoja kidogo tu!

114 Hiyo ndiyo sababu wakati mwingine watu hufikiria mimi hu—hu—huwa mkali kwa watu, kuwakemea, si kwa sababu siwapendi, ni kwa sababu kweli nawapenda. Vipi kama mvulana wako mdogo angekuwa ameketi nje mtaani, nawe ukasema, "Kadogoo, mpenzi, mimi—mimi—mimi. . . Hupaswi kuketi hapo nje. Baba hataki. . . "? Afadhali umchune ngozi, iwapo unampenda. Mwondoshe kwenye barabara hiyo. Upendo wa kweli hurekebisha, upendo wa kweli hurekebisha.

115 Vipi kama mke wako alikuwa akizurura huku na huko na mwanamume mwingine, nawe useme, "Mpenzi, na—natumaini una wakati mzuri, lakini kwa kweli sidhani unapaswa kulifanya"? Anapaswa kukufukuza *wewe* uondoke. Kweli. Naam. Upendo wa kweli hurekebisha. Na hiyo ni kweli.

116 Sasa, kutokuwa na uhakika. Makazi ya Marekani, siku hizi, hayana uhakika. Mtu kuoa mke, ha—hakika ni shida, bila shaka, ama mwanamke kuolewa na mwanamume, hakika ni jambo lisilo na uhakika. Hata wameliweka katika she—sherehe ya ndoa sasa, "Ninamchukua kwa heri ama shari." Kuna swali juu yake, halina uhakika. Ni bora kuliombea, sivyo? Nafikiri hilo lingekuwa bora zaidi, kuliombea kabisa. Lakini halina uhakika.

117 Nyumba zimevunjika, kufunga ndoa tena, kila mara wakati wote. Kutokuwa na uhakika wa maisha ya nyumbani. Marekani inauongoza ulimwenguni katika kesi za talaka, kati ya ulimwengu wote, Marekani inaongoza.

118 Biashara, kutokuwa na uhakika katika biashara. Hujui uanzishe biashara au la. Kuna ushindani mwingi sana, kuna mengi sana ya kila kitu, hujui uanze au la. Inatia shaka.

119 Na jambo lingine ni maisha ya kitaifa. Hatujui kama tujenge nyumba au la, inaweza kulipuliwa kabla ya asubuhi, huwezi kujua. Urusi imesimama pale, wana lu—lundo la makombora yaliyowekwa. Kitu pekee . . . Hawana haja ya jeshi, mtu mmoja tu aliyelewa vodka kidogo kupita kiasi kulifyatua, nasi tuwe mavumbi. Hamna njia . . . Yameelekezwa kila mahali. Ni hayo tu.

120 Pia kumbukeni, nasi tumewapangia vivyo hivyo, na kila kisiwa kidogo na kila taifa dogo wanayo. Haiwabidi kupigana vita vingine tena, kubonyeza tu kifyatulio nao wangetuma mabomu ya kutosha hapa, kusingekuwa na njia ya kulikomesha, huwezi kulikwepa. Watalipua shimo ardhini, wana hayo mabomu ya haidrojeni ambayo yatalipua shimo ardhini kwa kina cha yadi mia moja na hamsini, naamini ndivyo ilivyo, na maili mia moja na hamsini mraba (Ungewezaje kujiepusha nayo?) na maelfu yao yakingoja kulipuka kwa wakati mmoja. Ulimwengu usingeweza kulistahimili.

121 Nasi tunakimbia *kule* na kukunja ngumi zetu, nao wanakimbia *huku* tena, na kurudi nyuma mbio. Inatisha, kila taifa linaogopa. Hata afadhali . . . Kama vile, Ikulu ya Marekani, sisi ni kama mvulana mdogo usiku anayepitia makaburini, akipiga mbinja gizani, tukijifanya kama ni wakubwa na jasiri, lakini nyuma kote, kila mtu anatetemeka katika buti zake. Hakuna uhakika. Hiyo ni kweli.

122 Mkataba wa amani wa taifa letu, na chochote kile, kinatetemeka tu, U.N. inatetemeka, kila kitu kinatetemeka. Biblia ilisema ingetokea, ya kwamba kila kitu ambacho kingeweza kutikisika kingetikiswa. Lakini tunapokea Ufalme, usioweza kutikisika. Mnaona? Mnaona? Kila kitu kinatetemeka. Hakina uhakika.

123 Majira hayana uhakika. Hujui upande mazao yako wapi, usipokuwa na aina fulani ya umwagiliaji. Misimu, haina utaratibu kabisa, jalidi, mvua, chochote kile kinaweza kutokea kwenye majira ya kiangazi. Angalieni kile, wakati mmoja hapa walikuwa na mgando huko chini Florida mwaka jana, na wimbi la joto huko Alaska, hakuna uhakika.

124 Sayansi inasema dunia imevimba, ninasahau ni maili ngapi imevimba kuzunguka dunia, ikivimba katikati. Ufini ni karibu theluthi moja, au, moja katika nane kwa ukubwa kuliko ilivyokuwa miaka michache iliyopita, inapanuka, katikati ya dunia kunavimba. Loo, ndugu!

125 Ni nini? Se—selo nyekundu imeshushwa. Yeye anakuja, iweni tayari, Yuko moja kwa moja mlangoni. Hujui uende wapi upate usalama. Unanunua bima ya maisha. Unajuaje kwamba kutakuwa na maisha yoyote kutoka hapa, baadaye? Jinsi unavyofanya . . . U—unavyofanya kila kitu, lakini yote ni, ni kama kucheza kamari tu, hayana uhakika kabisa.

126 Maisha ya kanisa hayana uhakika. Makanisa, madhehebu, hayana uhakika kabisa, moja halijui la kulifanyia lingine. Hawana uhakika sana, mpaka wanajifunganisha pamoja, kisha wanaingia kwenye Baraza La Makanisa Ulimwenguni. Mtafanyaje hilo? mnapojichanganya na waaminio, wanaojifanya waaminio, na wasioamini, watu wanaokana kuzaliwa na bikira, wanakana ubatizo wa Roho Mtakatifu, wanakana uponyaji wa Kiungu, na kila kitu, na kujifunga nira miongoni mwa wasioamini, mkijaribu kufanya hivyo kwa ajili ya usalama.

127 Ati usalama? Mnajua, Biblia ilisema ngano na magugu yaachwe yakue pamoja, Naye angeyakusanya magugu mwishoni. Yanakusanywa. Yanakusanywa katika lundo moja kubwa mno, yote yanakusanywa kufanya sanamu ya mnyama, mamlaka ya kikanisa, sanamu kama Rumi.

128 Lo, inakuja, usijali. Itakuwa hapa, nanyi mtaiona; hamtakufa kwa uzee, hakuna mmoja wenu sidhani, mpaka mtakapoiona. Tuna kiongozi wake ameketi hapa sasa, Yezebeli, akigeuza shingo ya kila Ahabu, na . . . Mnakumbuka siku za huyo, sivyo? Ni wangapi waliowahi kusikia kanda yangu juu ya *Dini Ya Yezebeli*? Inatawanya lundo zima. Mnajua ninachozungumzia. Vema.

129 Sasa, kutokuwa na hakika, maisha ya kanisa, watu wa kanisa, hawana uhakika kabisa, watajiunga na Methodisti juma hili, "Je, hili ndilo?" wanaenda na kujiunga na Baptisti wiki ijayo, wanarudi kwenye *hili*, na hatimaye wanaishia katika Ukatoliki. Hiyo ni kweli. Bila uhakika! Hawajui pa kwenda. Wakatoliki wakikimbia *hapa*, na *pale*, na chochote kile. Hakuna anayejua la kufanya, kutokuwa na uhakika tu. Kitu hicho chote kinaonekana kuporomoka, hakina msingi.

130 Lakini je, kuna kitu ambacho ni cha hakika? Naam! Haleluya! Je, kuna kitu ambacho ni cha kweli? Hakika. Naam: Yesu alisema, "Mbingu na nchi zitapita, lakini Neno Langu halitapita kamwe." Hicho hapo kitu ambacho ni cha hakika. Naam, bwana. "Mbingu na nchi zitapita, lakini Neno Langu halitapita." Basi Hilo ni hakika.

131 Jambo moja la hakika, ni kwamba Neno la Mungu halitashindwa kamwe. Haijalishi jinsi wakosoaji wawezavyo kulikosoa vikali, jinsi *wasomi* wanavyoweza kulifafanua vinginevyo, jinsi wanavyoweza kufanya *hivi*, *vile*, ama *vinginevyo*, bali haitalikomesha hata kidogo, litatimia vivyo hivyo. Kama Yohana alivyosema, "Mungu anaweza katika mawe haya kumwinulia Ibrahimu watoto." Mungu atafanya jambo hilo, Maneno Yake yatatimizwa katika majira Yake, wala hakuna kitakachoweza kulizuia. Nina furahia sana hilo. Loo, jinsi nilivyo na furaha!

132 Paulo, hapa, alikuwa akizungumza katika Wakorintho 14:8, kuhusu kumfundisha askari, amezoezwa sauti fulani. Askari

huyo, kama yeye ni askari aliyefunzwa, anajua kila sauti ya baragumu hiyo kwamba afanye nini hasa, amefunzwa kwa baragumu hiyo. Wakati baragumu hiyo inapolia (Alisema, "Baragumu ikitoa sauti isiyojulikana," basi askari hajui la kufanya, kwa sababu amezoezwa tu sauti ya hiyo baragumu.), anajua kabisa la kufanya, kwa sababu sauti ya hiyo baragumu inamwambia la kufanya. Alisema, "Sasa, baragumu ikitoa sauti *isiyojulikana*," basi hajui la kufanya.

133 Sasa, hiyo ilikuwa ni kumfundisha askari wa kawaida. Naye askari Mkristo amefundishwa kwa Baragumu, sauti ya Baragumu, na hiyo ni Baragumu ya Injili, Injili, sauti ya Neno la Mungu, Baragumu ya Injili. Na kama mtu hakujua sauti ya Baragumu ya Injili, angechanganyikiwa kidogo. Kama hakujua kile Neno lilisema, na kile Neno lilifundisha, yale tu kanisa lilisema, angechanganyikiwa kidogo aliposikia sauti ya Baragumu, asingejua jinsi ya kujiweka tayari.

134 Nami nafikiri hapo ndipo tumefikia, ulimwengu leo hii, Baragumu inatoa sauti sawasawa na Injili, nao watu hawajui jinsi ya kutenda, hawajui jinsi ya kusimama mstarini na kujiweka tayari kwa vita. Wamechanganyikiwa kwa sababu wamekuwa wakisikiliza baragumu mbali mbali: kanuni za imani, madhehebu, umadhehebu, mambo ya kila namna, na wakati Injili ya kweli, pamoja na Neno la kweli lililodhihirishwa, limethibitishwa mle ndani watu hawajui la kufanya. Baadhi yao wanarudi nyuma, na kusema, "Ni—ni—ni ibilisi."

Huyo mwingine anasema, "Ni telepathia. Ni... Wamesisimkwa, hakuna kitu kama Roho Mtakatifu, Dk. *Nanii* alisema hivyo."

135 Sijali kile Dk. *Nanii* alisema. Mungu alisema nini? Hicho ndicho Kitu pekee kilicho imara, maneno yake yatashindwa, lakini Neno la Mungu halitapita kamwe, neno lake halina uhakika, lakini Neno la Mungu ni hakika. Hiyo ndiyo sababu ninajenga matumaini yangu si juu ya kitu chochote ila Biblia hiyo, haina budi kuwa hiyo.

136 Lakini ni ajabu, ninapoenda huku na huko na kuhubiri Neno, na kushuhudia mambo, labda kuchukua jambo rahisi, tamshi moja la Biblia, kwa kawaida ni bora kufanya hivyo, ningeweza kusimama hapa kwa majuma kadhaa na kupitia mambo na kuwaonyesha kwamba Maandiko yanaelekeza moja kwa moja kwenye wakati huu, wala hawaamini.

137 Sasa, hapa hivi majuzi usiku niliwakaripia ninyi wanawake kuhusu kuwa na nywele fupi. Je, mnajua Biblia inazungumzia hilo kwa ajili ya siku za mwisho? Hiyo ni kweli. Je, mnajua katika Biblia, ilikuwa ni kutotii kwa mwanamke kulikoanzishwa na wa kike, mwanamke huko nyuma, wakati jambo hili lilipoleta mauti kwa mara ya kwanza na wakati litakapoondolewa vivyo hivyo? taifa la Mataifa lililetwa na Mfalme Nebukadreza kwa

lugha zisizojulikana na kufasiri, na linaondoka kwa njia ile ile? liliingizwa kwa kuabudu sanamu ya mtu, na linaondoka . . . mtu mtakatifu, Danieli, ambaye alikuwa Belteshaza, sanamu ya Danieli, kumfanya kila mtu aabudu hiyo sanamu ya mtu mtakatifu, na kuondoka kwa njia iyo hiyo?

138 Mnajua, kila Andiko lina jibu maradufu Kwake, linajirudia? Hakika hujirudia. Nasi tuko katika siku hiyo. Jinsi tungeweza kuchukua saa nyingi juu ya hilo, na kuwaonyesha tu kwamba ni kweli kabisa! Nawe unaweza kuwaelezea watu, na kuwaonyesha watu, nao hawajui wapitie njia gani.

139 Mimi . . . Njia moja, unajisikia kama unataka kuwakemea, hata hivyo unawasikitikia, kwa sababu wamekuwa wakisikiliza kitu kingine ambacho ni kinyume. Lakini kila mara rudi uone kama ni BWANA ASEMA HIVI, kama ni Biblia, basi hilo ni la hakika. Na kila sehemu yake ni hakika, hata fungu moja dogo halitashindwa kamwe, kiasi cha mke wa Lutu kugeuza kichwa chake kwa watoto wake mwenyewe na wajukuu waliokuwa wakipiga mayowe, wakiungua katika Miali ya kuzimu. Ghadhabu ya Mungu na Hukumu ilimwagika juu ya Sodoma, naye huyo maskini mama huyo aliyehuzunika moyoni akageuza tu kichwa chake na kuangalia nyuma, lakini Malaika akasema, sasa, Malaika, mjumbe wa ule wakati kwa watu wao, akasema, "Hata usiangalie nyuma," naye akamwasi mjumbe huyo naye akageuza tu kichwa chake, naye bado amesimama leo.

140 Mnaona, marafiki, hiyo ndiyo shida, nimeiona miongoni mwa watu wetu, kamwe hatuna ule u—uaminifu, kile kicho na heshima kwa Neno hilo tunayopaswa kuwa nayo. Na hicho ndicho Kitu pekee kitakachosimama, ni hilo Neno.

141 Sasa, kama mtu hajui sauti ya Baragumu, hajui anachozungumzia, basi ni—ni . . . amechanganyikiwa kidogo. Sasa, siku hizi tunaona watu wamechanganyikiwa. Angalieni hapa, Wapresbiteri, Waepiskopali, Walutheri kwa mamia wanaingia wakimtafuta Roho Mtakatifu. Ajabu. Hiyo ni kweli. Mamia na mamia ya watu wa kimadhehebu wanaingia, wakimtafuta Roho Mtakatifu, nao Wapentekoste wanaopaswa kujua kinachotendeka, hawamtafuti. Badala ya kushika umati wa kusanyiko lao na kuwatikisa kwenye Injili, wanawaacha waendelee moja kwa moja kuishi kwa anasa kadiri watakavyo.

142 Wakati, hivi hamjui, Yesu alisema wakati bikira aliyelala alipokuja kununua Mafuta, ilikuwa ni saa iyo hiyo a—alipokuja Bwana arusi? Alipokuja, na kusema, "Hebu tupeni Mafuta yenu kidogo."

143 Kasema, "Tunayo tu ya kututosha sisi. Nendeni mkanunue." Basi wakati alipoenda kununua Mafuta, yule bikira aliyelala, ndipo Bwana-arusi akaja, naye Bibi-arusi akaingia. Sasa, hapajakuwa na wakati tuliopata kujua ambapo ulimwengu wa

kimadhehebu umekuwa ukimtaka Roho Mtakatifu hadi sasa hivi.

144 Ishara za Nuru ya jioni, maajabu, miujiza, kila kitu kimewekwa papa hapa tayari. Hakika. Wamechanganyikiwa kidogo. Hawajui. Kasema, "Loo, haleluya, haleluya! Wakiuendea moja kwa moja," na kuachilia kila kitu? Vema, tunapaswa kuwa tukichunguza. Ni wakati wa kwenda juu wakati hilo litakapotukia, wakati mwanamwali aliyelala alipoyalilia Mafuta.

145 Sauti ya Nuru ya Jioni inakuja. Sauti ya Nuru ya jioni ni nini? Kulingana na Malaki 4, ni Ujumbe wa kurudisha imani ya watu kwenye, ah, imani ya baba kuelekea watoto wao, Ujumbe.

146 Sasa, angalieni. Yesu . . . Kulikuwa na miti miwili katika bustani ya Edeni, mmojawapo ulikuwa Uzima, na mwingine ulikuwa mauti. Mmojawapo ulikuwa ni yule mwanamke, huo mwingine ulikuwa ni Mwanamume. Nao uhai unaotokana na mwanamke hufa, bali Uzima ule unaokuja kwa njia ya Mwanamume huishi. Yesu alisema, "Mimi ndimi Mkate wa Uzima ulioshuka toka kwa Mungu Mbinguni." Malaika . . . Maserafi waliulinda huo Mti wa Uzima, ambao ulikuwa ni Mkate wa Uzima uliotoka kwa Mungu Mbinguni, basi angalieni, ya kwamba hawangeula bila Upatanisho, ndipo ilibidi Upatanisho ufanywe, ndipo wangeweza kuula Mkate wa Uzima.

147 Huo hapo ule Mti mkamilifu, uliozaa tunda kamili, Daudi aliuona katika Zaburi na kusema, "Ni kama mti unaosimama kando ya mito ya maji." Hakika. Mito, mingi ya maji mamoja; karama nyingi, Roho yeye yule. Naye alizaa kila tunda kikamilifu, ndipo basi, Warumi wakamkata, wakamtundika juu ya mti uliotengenezwa na mwanadamu. Lakini aliporudi, Yeye aliweka, katika siku ya Pentekoste, aliweka nini? Mti wa Bibi-arusi pamoja na Roho Yake Mwenyewe katika Mti huo upate kuzaa tunda lile lile.

148 Ulijitokeza kwa miaka mia tatu ya kwanza, ukifanya vema. Ndipo madhehebu yakaingia ndani Yake, nalo kanisa Katoliki la Kirumi, siku hizi, lilikuwa ndilo Kanisa la kwanza la Kipentekoste. Kila ntu anayejua historia ya kanisa anajua hilo. Nimevisoma vyote hivi punde: *Waanzilishi Waliotangulia Nikea*, na *Baraza la Nikea*, *Baada Ya Baraza La Nikea*, *Babeli Mbili* cha Hislop, *Kitabu Cha Wafia Imani* cha Foxe, loo, *Nyakati Za Mwanzoni* cha Pember, vyote hivyo, nimevisoma vyote, nalo kanisa Katoliki la Kirumi lilikuwa ndilo Pentekoste ya kwanza.

149 Papa wa Katoliki ya Kirumi amesema hivi punde, "Makanisa yote, rudini sasa mahali makanisa yalipoanzia, huko Rumi." Ninataka msomi fulani, mwanatheolojia fulani, mwanahistoria fulani aniambie ya kwamba Kanisa lilianzia Rumi, ama, anionyeshe. Nitarudi pamoja naye mahali Kanisa lilipoanzia, lilianzia Yerusalemu, kwenye siku ya Pentekoste.

150 Sasa, nitakubali ya kwamba kanisa Katoliki, kanisa la *kimadhehebu* lilianzia Rumi. Madhehebu yalianzia huko Rumi, na huko ndiko yanarudi, maskini mama kahaba, na binti zake, ni kweli, atarudi kule.

151 Lakini Kanisa la asili lilianzia Yerusalemu, A.D. 33, kwenye siku ya Pentekoste. Huko ndiko ingetulazimu kurudi, ninajaribu kurudi huko. Lakini angalieni huo mwenendo wa mpinga-Kristo, ukijaribu kufanya mpinga-Kristo huyo, wakati Roho halisi wa Mungu akijaribu kuwarudisha kwenye imani ya asili tena? Angalieni hapo, "Yaliyosazwa na tunutu, yameliwa na madumadu; na yaliyosazwa na madumadu yameliwa na parare," kuendelea chini, chini mpaka unafikia kwenye kisiki. Yoeli aliuona, lakini akasema, "Nitarudisha, asema Bwana, miaka yote waliyokula."

152 Sasa, ilikuwa takriban miaka elfu moja pale, hapakuwa na kitu ila Kisiki. Lakini huwezi. . . Kwa sababu Uhai wa Mti huo umekusudiwa tangu zamani kuzaa Mti, akaja Luther, ukaufanya uanze kukua. Alifanya nini? Akaunda dhehebu. Yule Mkulima aliyapogoa matawi. Ukakua ukawa Methodisti. Ilifanya nini? Ikaunda dhehebu, kama tu mama yake. Matawi yakapogolewa. Ukakua ukawa Wapentekoste, ukafanya jambo lile lile, ukajiundia dhehebu. Mungu ameyapogoa hayo matawi.

153 Lakini Uhai huo ulio moyoni mwa Mti huo hauna budi kuishi, Mungu alisema, "Nitarudisha," kwa maana Nuru ya jioni ni ya—ya kuivisha. Katikati ya Mti huo kunasimama moyo wa Mungu, huo ni Mti wa Bibi-arusi kukutana na—na—na Mti wa Bwana arusi, kama tu ilivyokuwa katika bustani ya Edeni hapo awali, ule Mti, ile Miti miwili ya Uzima. Wachukue Adamu na Hawa kama—kama kivuli cha miti miwili ambayo kweli ilisimama pale, Uzima na mauti.

154 Na hapo ndipo inakwenda hadi leo. Loo, wamechanganyikiwa kidogo, hawajui la kufanya kuhusu hilo. Wanaposikia Baragumu ikilia, hawajui waendee njia gani, wanasema, "Vema, si—si—sijui." Linasikitisha, linahuzunisha. Hiyo ni kweli.

155 Makanisa ya siku Zake, hawakuijua hiyo Sauti. Angalia yale makanisa yalikuwa yamefanya: Walikuwa wa kikanisa, wenye elimu, werevu, wajanja, nao walikuwa wamezichukua amri zote za Mungu na kuzifanya mapokeo. Yesu alisema, "Mnazichukua amri za Mungu na kuzitangua kwa mapokeo yenu."

156 Walikuwa watu watakatifu, wenye haki, usingeweza kumnyooshea kidole mtu mmoja, angepigwa mawe kama angefanya jambo baya; babu wa babu wa babu zao walikuwa makuhani. Lakini Yesu akasema, "Ninyi ni wa baba yenu ibilisi." Ndipo Yesu alipokuja na kupiga Baragumu ya Masihi, hawakuijua, ilikuwa ni sauti isiyojulikana, hawakujua la kuamini.

157 Niaminini, ni jambo lile lile tena, limejirudia. Injili inatoa sauti katika usafi wa Neno Lake, na wa dhihirisho Lake, na bado hawalipati. Hawawezi kulielewa, hawajafunzwa Sauti hiyo ya Biblia. Wamefunzwa kanuni fulani za imani za kimadhehebu badala ya sauti ya Biblia, hivyo basi, Biblia inapoitangaza, hawajui unachozungumzia. Hiyo ni kweli. "Baragumu ikitoa sauti isiyojulikana, ni nani ajuaye jinsi ya kujiweka tayari?" Watu wanaendelea tu, wanaishi kama tu wengine, lakini laiti wangeweza tu kuiona hiyo Sauti: Mungu akitenda kazi!

158 Niliingia India, hapa siku moja, mimi na Billy, tulipoenda India, ambako tulikuwa na mkutano wetu mkuu sana tuliowahi kufanya, ilikuwa huko Bombay, ulio mkubwa kuliko yote, nami nadhani kulikuwa na, sijui, labda kulikuwa na laki moja, watu laki mbili walimpokea Kristo kwa wakati mmoja. Hatukujua jinsi tungeweza kuwadhibiti, kama tu maili nyingi za mikono myeusi ikiinuliwa juu, wakimkubali Kristo wakati kipofu kabisa jukwaani alipofunguliwa macho, akaponywa. Na hao hapo.

159 Lakini kwa sababu hakuna makanisa yangeshirikiana nao, basi walifanya nini? Wakati ha—ha—ha—hawakuielewa vizuri Sauti ya Injili! Wakati askofu huyo wa Methodisti aliposimama pale, naye akaniambia, akasema, "Bwana, tunaamini wewe ni mtu wa heshima, hatukubaliani nawe. Una jina zuri, tunakuheshimu. Lakini kukufadhili . . . "

160 Nikasema, "Bwana, mtu fulani hana budi kuchukua huko nje. Huyu hapa meya amesimama hapa, ambaye aliniambia kwamba kulikuwa na angalau, kutakuwa na angalau watu laki tano katika kusanyiko hilo." Nikasema, "Jambo fulani litatokea. Ingieni ndani na kuwachukua watu hao, muwaongoze kumjua Kristo, hata kama ni kwa Kitabu tu."

161 Lakini mnaona, Baragumu ilipigwa kwa ajili yao, bali wao . . . Ilikuwa ni sauti isiyojulikana kwao. Hawakujua, hawakujua hiyo Baragumu ya Injili, mnaona. Walijua tu baragumu yao ya taratibu, baragumu yao ya kikanisa, hayo ndiyo yote waliyojua, wakaipoteza. Nao watawajibika kwayo kwenye Siku ya Hukumu. Hiyo ni kweli kabisa.

162 Yesu alipiga Baragumu Yake, akawaonyesha kwa ishara na maajabu Yake ya kwamba Yeye alikuwa ndiye Masihi. Naam, bwana. Askari Mkristo amefunzwa kusikia Neno-Sauti ya Injili, askari Mkristo halisi amefunzwa Hiyo. Yesu alisema, "Kondoo Wangu wanaijua Sauti Yangu." Sauti ni nini? Yesu ni Neno, "Hapo mwanzo alikuwako Neno, huyo Neno alikuwa pamoja na Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno alifanyika mwili, akakaa miongoni mwetu." Basi kondoo halisi wa Mungu huisikia Sauti ya Neno. "Kondoo *Wangu* huisikia Sauti *Yangu*. Na mgeni hawamfuati." Mwalipata?

163 Kanuni za imani na mafundisho ya sharti, na kadhalika, zinaingizwa ndani Yake. Hawatafuata hayo, hawana budi

kulisikia Neno lisiloghoshiwa, na kuliona likidhihirishwa. Angalieni tu kidogo hapa katika Injili katika dakika chache, muone kama ndivyo au sivyo. Walifika kwa: "Kondoo Wangu huisikia Sauti Yangu."

164 Angalieni, Israeli wote, katika makumi ya maelfu waliokuwako katika siku hizo, takriban milioni nne, na kulikuwa na mia moja na ishirini walioisikia Sauti Yake, kati ya milioni nne. Kama unyakuo ungekuja usiku wa leo, ingetisha sana kama ningewaambia kile ninachowazia kingetukia. Ni kweli.

165 Kuna mengi, kama nilivyomwambia ndugu mmoja asubuhi ya leo, kuna mengi ya yale *yanayoitwa* Ukristo yamechanua kote duniani, ni kijazio tu bustanini kinachoelekeza kwenye Sanamu. Sanamu ndicho kitu cha kuangalia, Kristo ndiye Sura hiyo. Kweli. Nalo Kanisa la kweli lililozaliwa mara ya pili ndilo atakalochukua pamoja Naye, mengine yote ni kijazi. Hiyo ni kweli.

166 Sasa, kanisa halikumfahamu. Kwa nini? Kwa sababu hawakuwa . . . walikuwa wamefunzwa sauti ya mifumo ya kikanisa ya siku hizo. Ilikuwa ni sauti isiyojulikana. Hawakujua la kufanya wakati Yesu alipojitokeza pale na kubashiri mambo, na kutabiri mambo, na hata hivyo Maandiko yao wenyewe yakiwaambia ya kwamba atakapokuja hivyo ndivyo angefanya.

167 Lakini walikuwa wamefanya mapokeo kutoka Kwake, na kusema, "Vema, Masihi atakuwa *hivi-na-hivi*. Sasa, Dk. *Nanii* na Rabi *Nanii* walisema, '*Hivi-na-hivi*.'" Mnaona, kuchukua neno la mwanadamu, halina hakika, bali Neno la Mungu ni kweli halisi.

168 Mungu alisema kupitia kwa Musa, nabii Wake, nalo Neno sikuzote humjia nabii, na kusema ya kwamba angekuwa nabii kama yeye, nao walikuwa wakitazamia hilo. Na wale waliolitazamia walilipokea. Mnaona? "Kondoo Wangu wanaijua Sauti Yangu."

169 Lakini siku hizi . . . Siku hizo ilikuwa ni watu wa kanisa wa siku Zake walioelimishwa wenye mafunzo, hawakuijua hiyo Sauti. Walikuwa ni watu wazuri, usingeweza kuwakamata. Usingeweza kusema walifanya uzinzi, walisema uwongo, waliiba, walifanya *hivi*. La, bwana. Usingeweza kusema hawakuwa werevu, walikuwa na akili nyingi, werevu tu kama walivyoweza kuwa.

170 Lakini hawakuijua hiyo Sauti, wala hawakujua la kufanya. Walichanganyikiwa. Loo, jinsi ningeninii . . . Nashikilia tu kitu fulani, ningependa kuwalipua. Nena kuhusu kuchanganyikiwa! Naam, kuchanganyikiwa, hawakujua la kufanya. Waliona jambo fulani likitukia, nao walijua iliwabidi kuwajibika kwa watu wao, na badala ya kuichukua Injili na kuichunguza, wakati aliposimama pale na kuyatambua mawazo yao, na Yeye . . . wakasema, walikuwa wanaenda kuwaambia watu wao kwamba

Yeye alikuwa Beelzebuli. Walilitupilia mbali tu na kusema, “Loo, ni la ibilisi.”

171 Yesu akageuka, akasema, “Nimewasamehe hilo, lakini siku moja Roho Mtakatifu anakuja kufanya jambo lile lile, na neno moja dhidi Yake halitasamehewa kamwe.”

172 Kutokuwa na hakika, na uhakika: Wakati Sauti ya hakika inaponena, isiyo ya hakika huchanganyikiwa, na wakati isiyo na uhakika inaponena, iliyo hakika inachanganyikiwa mpaka aone aliponinii...kile kinachonena. Naam. Mtu anayejua mahali anaposimama, anaweza kusikia ni nini...kusikia sauti isiyojulikana, lakini hataisikiliza, na hiyo ni kweli, “Mgeni hawatamfuata.”

173 Vema. Ilikuwaje? Ni nini kilichowafanya kuwa hivyo? Walifanya nini? Walifanyaje? Walilikana Neno. Na unapolikana Neno, kuna jambo moja tu la kujengea, na hilo ni mfumo wa elimu. Ukweli unapokataliwa, elimu inakubaliwa. Hiyo ni kweli kabisa. Walichukua elimu; jambo lile lile leo.

174 Angalieni makanisa yetu ya Kipentekoste, ndugu. Sasa, afadhali tuyafungue macho yetu na kukabiliana na ukweli. Makanisa yetu si kama vile yalivyokuwa. Sasa, makanisa yenu ni ndugu zangu. Mimi...Wako sawa, ninawapenda. Hiyo ndiyo sababu niko pamoja nao. Kama sikuwaamini, hakika nisingekuwa hapa nikisema ninachosema. Ninawapenda. Lakini imekuwaje? Badala ya yale matukio tuliyokuwa tukipata na Mungu, tunawapeleka watoto wetu hapa shuleni mahali fulani, na kupata Ph.D. na LL.D., kisha tunamleta nyumbani, yeye hajui zaidi juu ya Mungu kuliko Mhottentoti anavyojua kuhusu hekaya za Kimisri. Kweli.

175 Tunawapeleka watoto wetu...katika shule za Jumapili. Mungu hana wajukuu wowote, Mungu ana wana. Hiyo ni kweli. Lakini tunawaingiza, kasema, “Vema, wao ni Wapentekoste kwa sababu mama yao alikuwa Mpentekoste na akawalea Kipentekoste.” Hilo haliwafanyi kuwa Wapentekoste.

176 Mungu hana wajukuu wowote, Yeye ana wana na binti tu, sio wajukuu wa kike wala wajukuu wa kiume. Yeye ana wana na binti pekee. Maskini huyo Riki hana budi kulipa gharama ile ile ambayo babu alilipa, kufanya jambo lile lile alilokuwa nalo babu, apate tukio lile lile walilopata babu na nyanya, asipolipata, amepotea.

177 Usigeuze kichwa chako kuangalia nyuma, endelea kwenda mbele. Usiuangalie ulimwengu, na baadhi ya mambo haya ya kimtindo, na baadhi ya mikono hii iliyojaa mambo ya kimadhehebu wanayoeneza. Sisi sote tuna hatia. Hiyo ni kweli, hatuijui Sauti hiyo inayojulikana. Tunakubali mafundisho madogo ya sharti na kuyashika.

178 Yesu, alipokuja, hata asingeweza kupata yeyote kati yao. Aliwachukua wavuvi, mtu ambaye hakujua chochote ambacho

Yeye angeweza kuonyesha kitu kwacho. Naam, bwana. Katika Timotheo wa Kwanza mlango wa 14, kunradhi, Timotheo wa Kwanza, mlango wa 4, inasema ya kwamba katika siku za mwisho, Roho Mtakatifu ananena, kwamba kungekuwa na dhana ya kiakili ya Kanisa. Hiyo ni kweli.

179 Timotheo wa Kwanza mlango wa 4 ilisema, "Jueni jambo hili: Roho Mtakatifu anena ya kwamba katika siku za mwisho," hizo ni siku hizi, mnaona, "watakuwa wakaidi, wenye kujivuna, wapendao anasa kuliko kumpenda Mungu, wasiotaka kufanya suluhu," (Ilikuwa ni aibu kwa—kwa wanawake kwenda kuoga pamoja na wanaume, sasa ni jambo linalopendwa sana; wao ni Wapentekoste, hakika, mnaona. Vema.) "wasiotaka kufanya suluhu, wasingiziaji, wasiojizuia, na wasiopenda walio wema."

Unasema, "Ndugu Branham, hao ni wakomunisti."

180 Hao walikuwa washiriki wa kanisa. Angalia alichosema baadaye: "Wenye mfano wa utauwa," hao walikuwa ni Wapentekoste, wanaweza kupaza sauti, kurukaruka, kunena kwa lugha, kukata nywele, kuvaa nguo za kizinifu, wahubiri wanapita na kuwaweka watu kanisani, mashemasi walio na wake wanne ama watano, na chochote kile. Pesa tu na mavazi, na umaarufu, kuwaleta walio bora kuliko wote mjini, jamii ya mjini.

181 Walio bora kuliko wote mjini, wakati mwingine, wako kwenye maskani ya wasokwao, kama ni Mungu, mwanamke au mwanamume mwenye moyo mnyofu anayetaka kumtumikia Mungu. Angalieni katika wakati wa Biblia, baadhi ya walio bora zaidi waliokuja walikuwa ni akina Mariamu Magdalene, ambaye Yeye alimtoa pepo saba, na kadhalika. Tunaanza kuhangaika, wenye kujivuna.

182 Hiyo ndiyo sababu tunapoteza, kwa sababu tunawachukua wavulana wetu na kuwafundisha elimu, badala ya kanuni za Biblia, na wokovu wa Mungu, na nguvu za Roho Mtakatifu. Hiyo ndiyo sababu kwenye uamsho huu mkuu, tumefanya nini? Assemblies imeangua kundi kubwa sana, kama vile Oral Roberts; lile lingine, Church of God; Billy Graham, Wabaptisti, na kadhalika, maelfu na maelfu. Lakini liko wapi lile Kanisa ambalo Kristo alinena habari zake? Ziko wapi zile nguvu kuu za Mungu alizoahidi?

183 Kuamini kwa mpakani. Israeli walikuwa jangwani miaka arobaini, wakitembea kote na baraka za Mungu, lakini ndugu, huko kwenye nchi ya ahadi kulikuweko na utimilifu wa baraka za Mungu kwa ajili yao. Nasi siku hizi tunazunguka-zunguka katika duara, namna hiyo, huku nguvu za Mungu zikiwa tayari kutuingiza ndani, pia, lakini tunafanya nini? Kupanda mbegu za kiakili, mazungumzo ya kiakili, hakuna mikutano ya maombi tena ya usiku kucha, inabidi kuharakisha na kuondoka. Uaminifu umetoweka. Yako wapi mambo hayo? Basi acha

Mungu ainue kitu fulani, halafu wanakikosoa, Kanisa la Mungu aliye hai. Wazieni hilo. Sauti isiyojulikana, hawaijui. Hakika. Vema.

184 Alizungumza juu ya jambo hili, sikilizeni yale aliyosema, pia, katika Timotheo wa Pili, Yeye alisema, "Hawa wangekuwa ndio aina ya wale waendao nyumba hata nyumba, na kuwachukua mateka wanawake wajinga, wanaochukuliwa na tamaa nyingi. Bila kujifunza, wasioweza kuufikia ujuzi wa ile kweli, wenye kulemewa na dhambi, tamaa." Unataka kuiga nyota fulani wa sinema, kipindi fulani cha televisheni ulichokaa nyumbani pasipo kuhudhuria mkutano wa maombi upate kukitazama, ukimfanya huyo mfano wako.

185 Nusu ya watoto wanaweza kukwambia zaidi kuhusu Davy Crockett kuliko wanavyoweza kuhusu Yesu Kristo. Hebu shuka uende katikati ya mji, unaweza kununua chochote kutoka kwa Davy Crockett, lakini ni vigumu kusikia Jina la Yesu Kristo likitajwa. Loo, ni aibu!

186 Najua mnafikiri mimi ni mwendawazimu, lakini baadhi ya siku hizi kwenye Kizimba cha Hukumu, nitakaposimama pale karibu nanyi, mtaona vinginevyo. Sasa ndio wakati, msingoje mpaka kule, itakuwa imechelewa kupita kiasi. Lihukumuni kwa Neno, muone kama ni kweli. Kisha mtajua.

187 Kiakili, hawatataka mtu fulani asimame hasa na kuyafungua Maandiko na kuyaonyesha, wanataka mtu ambaye amefunzwa kuyakwepa. Hawataki kujua hilo. Loo, kamwe hawawezi kustahimili hilo.

188 Samaki na mikate ni sawa, lakini . . . Yesu alifanya jambo lile lile. Ni Nabii wa ajabu jinsi gani! Maskini yule Nabii wa Galilaya alikuwa akiwaponya wagonjwa, Naye alikuwa Mtu mashuhuri, lakini siku moja aliketi chini, akaanza kuwamiminia kweli. Kundi zima likaondoka na kumwacha, hata wale sabini wakaondoka, ndipo akawageukia wale kumi na wawili na kusema, "Je, mnataka kwenda pia?"

189 Hapo ndipo Petro alipotoa maneno yale mashuhuri, na kusema, "Bwana, twende wapi?" Bila shaka. Ndipo akaanza tangu saa iyo hiyo (Maadamu alikuwa akiwaponya wagonjwa, ilikuwa sawa, lakini alipoanza kuingilia maisha yao binafsi, basi hilo lilisema jambo tofauti.) tangu papo hapo Huduma Yake ikaanza kupungua, moja kwa moja mpaka msalabani. Na kila mtumishi wa kweli wa Mungu atafuata mfano huo, bila shaka. Watu wanapenda kubembelezwa na kuchezewa, lakini inapofikia ukweli, hawautaki. Sasa, kumbukeni, hizi ni kanda zinazosambazwa ulimwenguni kote. Mnaona? Sawa.

190 Elimu, ningesema hivi, kwamba elimu imekuwa mojawapo ya mambo ya kuchukiza sana ambayo Injili imewahi kupokea. Na siku hizi elimu ni ya lazima. Hiyo ni kweli. Huna budi kuwa nayo. Waangalie watoto wa Kaini, hapo mwanzo, watoto

wa Kaini walikuwa werevu, wanasayansi, na wa-. . . na—na wangeweza kutia chuma matiko, kujenga mijengo, na kadhalika, walikuwa wanasayansi. Lakini watoto wa Sethi walikuwa wachungaji wanyenyekevu na kadhalika. Hiyo ni kweli.

191 Yesu alisema watoto wa ulimwengu, wa usiku, ni werevu zaidi, wana akili kuliko watoto wa mchana, Yesu alisema hivyo, na hata hivyo, tunaweka mengi sana juu ya hiyo akili. Mtu fulani anayeweza kusema "Aa-mina" vizuri kabisa, mtu fulani mwenye nywele mtindo wa Hollywood, ama *kitu kingine*, "Anaongea vizuri sana," kuoga kwa mchanganyiko, kutoka nje, na kufanya kila kitu, kucheza kamari kanisani, na karamu ndogondogo za kijamii na kadhalika, na hata mngempigia kura mtu kama huyo awe mchungaji wenu.

192 Paulo alisema alitaka watenganishaji. Mungu alimwambia Paulo, "Nitengeeni Paulo na Barnaba." Leo wanataka wachanganyaji, kuwaacha wapite na lolote wanalotaka, lakini Mungu anataka watenganishaji. Hiyo ni kweli. Si rahisi kufanya, lakini hata hivyo, ni kutimiza kile ambacho Mungu anataka.

193 Kondoo wanazoezwa kuifuata Sauti ya mchungaji, nayo Sauti ya mchungaji ni Neno. Siku hizi elimu ni mashuhuri sana, ni ya lazima. Moja ya makusanyiko yetu makuu, mojawapo ya madhehebu yetu makubwa zaidi ya watu wa Full Gospel, ninaambiwa, inawabidi kumchukua mmishenari na kumsimamisha mbele ya daktari wa akili waone kama yuko sawa kiakili kwenda hudumani au la. Ni fedheha jinsi gani!

194 Siku hizi inakubidi kuwa na digrii nne hivi chuoni, au, digrii mbili kabla hata hawajakuweka wakfu kuihubiri Injili. Inakuchukua miaka kumi kwa namna fulani ya digrii. Mungu alifanya zaidi katika siku kumi kuliko wanavyoweza kufanya, siku hizi, katika miaka kumi. Hiyo ni kweli. Watu ambao hata wasingeweza kuandika majina yao wenyewe! Kamwe hakuwaambia waende shuleni. Yeye. . .

195 Wakati (naamini ilikuwa ni Hudson Taylor, yule mmishenari mkuu huko Uchina.), kulikuwa na mvulana Mchina aliyeokoka, kisha akaja, kasema, "Bw. Taylor, nitapata wapi Digrii yangu ya Sanaa? *Hii* itachukua miaka mingapi? Itachukua miaka mingapi, kupata digrii yangu ya uzamifu?"

Bw. Taylor akasema, "Nenda sasa, usingoje hadi mshumaa umeungua nusu."

196 Ndivyo ninavyosema leo hii. Tunachohitaji leo ni watu wenye ujuzi wanaojua kile Mungu anamaanisha, na wanachukua ujuzi wa Mungu kwa Biblia ya Mungu, na kulihubiri Neno la Mungu, wenye ishara za Mungu, na thibitisho la Mungu.

197 Ikiwa hujui maharagwe kutoka. . . kutofautisha maharagwe na kahawa, hubiri kwa vyovyote vile. Kuna jambo moja unalojua: Kama mshumaa wako uliwashwa, nenda kamwambie mtu fulani jinsi ulivyowashwa, labda wao pia utawashwa,

uwashwe kutokana na wako. Hilo ndilo tunalohitaji siku hizi. Ndivyo hakika. Tuna wataalamu wengi kupita kiasi wa magonjwa ya akili, na mambo mengi sana tunayopaswa kufanya katika nyanda za elimu. Naam, bwana.

198 Mungu alifanya maagano mawili, matatu. Agano la kwanza alilofanya, alilifanya pamoja na Adamu, akalivunja. Agano la pili lilikuwa agano la Nuhu, likavunjwa. Mungu alipofanya agano Lake na Ibrahimu, hakusema kamwe, "Ikiwa utafanya mambo *fulani*, nitafanya mambo *fulani*." Alisema, "Nimefanya!" Agano lisilo na masharti, Mungu aliamua kumwokoa mwanadamu. Hakuna ishara isiyojulikana kuhusu hilo. "Ibrahimu, nimekuokoa wewe pamoja na Uzao wako baada yako, nami nitaapa kwa nafsi Yangu kwamba nitalitimiza." Amina. Hakuna kitu kisichojulikana kuhusu hilo. "Nimelifanya, tayari nimelifanya." Mnaona, kwanza kabisa mwanadamu ameoza, chochote afanyacho kimeoza, chochote afanyacho.

199 Ndugu mmoja nyuma hapa kanisani, nilikutana naye hivi majuzi asubuhi, gari lake, sote wawili tulinunua Ford mpya, nasi tuliposhuka huku, mbona, yangu iliharibika, yake ikaharibika, Billy alinunua Chevy mpya nayo ikaharibika, nami nikasema, "Kitu chochote anachojenga mwanadamu kinaweza kuharibika. Kuna Kitu kimoja tu kisichoharibika, hicho ni Kristo." Amina. Anaishi milele.

200 Nuhu alivunja agano lake, au, agano la Nuhu lilivunjwa, agano la Adamu lilivunjwa, chochote ambacho Mungu hufanya na mwanadamu. Lakini Mungu alidhamiria, naye angemwokoa mwanadamu, kwa sababu alimjua mwanadamu tangu zamani. Naye alidhamiria kumwokoa, hivyo akamwokoa mwanadamu kwa agano lisilo na masharti. Amina. Hakuna shaka juu yake, alisema, "Nitafanya." Ni kwa neema kabisa, na bila masharti, ambalo linaifanya kwa neema. Sio, "Ukifanya, nitafanya." Loo, jinsi ninavyofurahia hilo! Si kile nilicho, bali kile Yeye alichokuwa. Amina.

201 Ibrahimu, aliposikia agano hilo, alifurahi sana na kushangilia, hata akiwa mzee, naye Mungu akamwambia atapata mtoto kwa Sara. Miaka ikapita, wala hakumpata huyo mtoto, lakini akaendelea kusema, "Tutampata kwa vyovyote vile."

"Unajuaje?"

202 "Mungu alisema hivyo." Hakuna shaka kuhusu hilo. "Tutampata kwa vyovyote vile, Mungu alisema hivyo, hilo latosha." Mungu alisema hivyo, hakuna shaka juu yake.

203 Nuhu, Ujumbe wake siku hiyo haukukidhi elimu ya kanisa. Mnakumbuka walikuwa watu werevu zaidi wakati huo, walivyo sasa. Wangeweza kujenga piramidi na sfiniksi, wasingeweza kufanya hivyo sasa, hatuna kitu cha kuyanyanyua hayo huko

juu, hayo majabali. Ni kweli. Wangeweza kutengeneza mumiani katika siku hizo, au kutia mwili dawa usioze kuufanya udumu mamia na mamia ya miaka uonekane wa kawaida, tumepoteza ustadi huo. Walikuwa na rangi ambayo hatuna siku hizi. Walikuwa werevu zaidi wakati huo, kuliko tulivyo sasa.

Unaonaje mzee fulani akienda huko na kusema, "Vema, jiandaeni, ninaenda kujenga safina hapa nje kwa sababu mvua itanyesha"?

204 Wanasayansi wangeirusha ninii . . . rada mwezini na huku na huko, kasema, "Siyo tena . . . mvua yoyote kati ya huku na kule. Inatoka wapi?"

205 Kama yule Mrusi kwenye mzingo hivi majuzi, alisema, "Niliizunguka dunia mara kumi na saba, sikumwona Mungu yeyote, wala Roho Mtakatifu, wala malaika." Ujinga, hivyo tu. Mungu huketi tu na kuwacheka.

206 Mbona, Ujumbe wa Nuhu haukustahili maelezo ya kisayansi, lakini Nuhu alisema, "Mvua itanyesha," kwa vyovyote vile, maana Mungu alisema hivyo. Naam, bwana. Hakuna sauti isiyo dhahiri hapo. "Mvua itanyesha."

207 Musa alikuwa anahojiwa, nabii huyo mtoro huko nje upande wa nyuma ya jangwa, hakujua la kufanya. Loo, alikuwa amehangaika sana. Kasema, "Bwana, siwezi kuzungumza, nina kigugumizi, si—siwezi kufanya hivyo, siwezi kushuka kwenda huko."

208 Lakini Mungu aliposema, "Nitakuwa pamoja nawe," Amina. Hakuna sauti isiyojulikana hapo. "Nitakuwa pamoja nawe." Amina. Hilo lilitosha. Musa alishika njia, hakuna shaka kuhusu hilo.

209 Daudi, aliposimama pale karibu na Goliathi, akimwangalia, na kuona kundi hilo la askari wa bati, wanaodhaniwa kuwa ni jeshi la Mungu, wamesimama pale, waoga, wakirudi nyuma, Daudi alisema, "Mungu aliyemtia simba mkononi mwangu, kisha nikamwua dubu, Mungu yuyo huyo atamtoa Mfilisti huyo asiyetahiriwa mkononi mwangu." Sasa, sio, "Natumaini atafanya hivyo. Pengine Yeye atalifanya." Alisema, "Atafanya hivyo." Hakuna shaka lolote hapo.

210 Kuna Sauti iliyo hakika, na Sauti fulani hiyo ya hakika ni Sauti ya Mungu. Haleluya! Hakuna shaka kuihusu hiyo. Daudi alisema, "Atafanya hivyo."

211 Yohana alikuwa na hakika sana, huko nje katika nyika ile, kwamba angemwona Yesu Kristo, alikuwa na hakika sana angemwona, akasema, "Yeye amesimama katikati yenu sasa, wala hamumjui." Alikuwa na hakika. Sio, "Natumaini yuko huko nje. Labda atakuja wakati ningali hai."

212 Yohana alikuwa na Ujumbe moja kwa moja kutoka kwa Mungu. Hakwenda shule kujifunza chochote, alienda nyikani

kwenye magoti yake. Ujumbe wake ulikuwa muhimu sana asingechukua wazo la shule. Kwa hiyo akaenda mpaka akamwona Mungu, naye Mungu akamwambia, kasema, "Ambaye utamwona Roho akishuka na kukaa juu Yake, Huyo atabatiza kwa Roho Mtakatifu na Moto."

213 Yohana alikuwa na uhakika nalo. Kwa hiyo alikuwa na uhakika sana akasema, "Amesimama miongoni mwenu sasa, Mmoja ambaye hamumjui." Amina. Alikuwa pale, lakini hakuwa amejidhihirisha Mwenyewe bado.

214 Jinsi ningependa kusema jambo fulani hapa! Amina. Ninaamini Yuko hapa, lakini bado hajajidhihirisha Mwenyewe. Ninaamini Kristo yuko hapa, ninaamini katika umbo la Roho Mtakatifu, Yuko papa hapa sasa katika utimilifu wa uwezo Wake kufanya lolote tunalomwomba afanye; Alisema hivyo. Lakini atakapojidhihirisha Mwenyewe, kumbukeni, ataonekana kabla hajaja. Lakini tutamwona akija moja ya siku hizi, Yule mtukufu ambaye tumemtazamia. Naam. Amina.

215 Yesu alikuwa na uhakika na kile alichofanya. Katika Yohana Mtakatifu mlango wa 5, kifungu cha 19, Yesu alisema, "Amin, amin, nawaambia, Mwana hawezi kutenda neno Mwenyewe," huo ni mwili ambao Mungu aliumba, Mwanawe Mwenyewe. Je, mnaamini Yeye alikuwa Mwana wa Mungu, aliyeumbwa? Hakika, naam. Mungu alijiumbia Mwenyewe mwili, maskani, apate kuishi ndani yake, alikuwa Mwana wa Mungu, Naye akasema, "Mwana hawezi kutenda neno Mwenyewe, ila lile amwonalo Baba analitenda, ndilo atendalo Mwana vile vile." Ndipo alikuwa na uhakika, kwa sababu Mungu alikuwa akimwonyesha la kufanya. Alikuwa na hakika Mwenyewe. Loo!

216 Jinsi Eliya alivyokuwa na hakika! Akatoka pale na kuwakata hao maksai na kuwaweka huku na huku kule chini, akawaambia, "Mwiteni mungu wenu, Baali." Kasema, "Endeleeni, mwiteni muda mrefu zaidi, labda anawinda, labda yuko kwenye safari ya uvuvi mahali fulani, labda ndio kwanza apate shida ya kusikia," akatembea huku na huko pale. Kwa nini? Walisema, "Maana, loo, yeye ni mtu wa imani." Yeye ni mtu, aliona ono. Hakuna mtu aliyefanya jambo lolote pasipo kuliona kwanza katika ono, Yesu hakuwahi Mwenyewe, alisema hakuwahi.

217 Lakini alisema nini? Alipowaweka wote huko nje, alisema, "Bwana, nimefanya haya kwa amri Yako." Amina. Alikuwa na uhakika. Kasema, "Sasa, Bwana, jalia ijulikane ya kwamba Wewe ndiwe Mungu, nami ni nabii Wako." Ndipo Moto wa Mungu ukaanza kushuka kulingana na unabii wake: "Hebu Mungu anenaye kwa Moto ajibu." Hakuna shaka kuhusu hilo, alijua alichokuwa akifanya.

218 Hebu Mungu aliye Mungu anene kama Mungu. Hebu Mungu anayejibu kwa Moto awe Mungu. Hebu Mungu usiku wa leo . . .

Ikiwa mifumo yenu ni bora kuliko Neno, basi na inene na kuwaponya wagonjwa, na kuyatambua mawazo, na kufanya yale ambayo Mungu alisema angefanya. Amina. Mifumo yenu ya kimadhehebu ikiwa ni bora kuliko Neno la Mungu, basi hebu inene. Hebu tuwaone wakiinua kanisa katika mafundisho yao ya sharti ya Kirumi, na kadhalika, na kutoa kitu kama Yesu Kristo. Hebu tuwaone na mafundisho ya sharti wakilifanya Neno liishi tena.

219 Wanalikwepa Neno kwa mafundisho yao ya sharti, kanuni yao ya imani siku hizi, kwa sababu wanaogopa kukabiliana na suala hilo, kisha wanalikwepa na kuwawekea watu msingi juu ya elimu ya kiakili badala ya uwezo wa kufufuka Kwake Yesu Kristo, na dhihirisho la Utu Wake. Amina. Hakuna shaka kuhusu hilo. Lijaribu. Bila shaka ni kweli. Naam, bwana.

220 Yesu alisema, "Sifanyi lolote mpaka Baba anionyeshe." Naam, bwana. Yesu alikuwa na uhakika sana na Huduma Yake hata akasema, "Yachunguzeni Maandiko," sasa, mtu hatasema hivyo. "Yachunguzeni Maandiko; kwa kuwa ndani yake mnadhani mna Uzima wa Milele, na Hayo Ndiyo yanayonishuhudia Mimi."

221 Kwa maneno mengine, "Je, hamjui ya kuwa Mimi ni Neno? nami niko hapa kudhihirisha Neno lililoahidiwa? kile ambacho Mungu aliahidi kwamba Masihi angefanya, mimi niko hapa kukithibitisha?"

222 Mbona si lile kanisa la Kipentekoste, usiku wa leo, basi? Kazi zile zile ambazo Mungu aliliahidi Kanisa kufanya, tunapaswa kusimama kwa miguu yetu katika Jina la Yesu Kristo na kuzifanya.

223 Wakati Eliya, yule nabii mzee, aliyemwakilisha Kristo, Elisha, yule nabii kijana, alimfuata kuvuka Yordani, aliporudi, alikuwa na sehemu maradufu. Nalo Kanisa lilimfuata Kristo hadi Kalvari, ndipo vazi la Kristo likaanguka chini pamoja na ubatizo wa Roho Mtakatifu. Naye Yesu akasema, "Mambo haya niyafanyayo ninyi nanyi mtayafanya; na hata makubwa kuliko haya mtayafanya," mengi zaidi, "kwa sababu Mimi naenda kwa Baba Yangu." Amina.

224 Yuko wapi Mungu wa Yesu Kristo? Yuko wapi Mungu aliyetoa ahadi hii katika Biblia? Tunahitaji Elisha wengine zaidi. Kweli. Tunahitaji waaminio zaidi katika hilo. Tunahitaji wengine zaidi wanaoamini ukweli, kwa sababu kumekuwako na kanuni nyingi za imani zilizopotoshwa na kadhalika, ni—ni sauti isiyo dhahiri kwa watu.

225 Ninajaribu kuwaambia, rudini kwenye Biblia. Msiache mtu yeyote awaambie siku za miujiza zimepita. Msiache mtu yeyote awaambie Roho Mtakatifu si yule yule tu kama alivyowahi kuwa. Msiruhusu mtu yeyote awaambie kwamba Yesu Kristo hayuko hai, na yuko papa hapa katika Kanisa Lake usiku wa

leo, akifanya mambo yale yale aliyofanya. Hakuna shaka juu ya hilo, aliliahidi.

226 Lakini watu pamoja na upuuzi wao wa kikanisa, wanaanza kufikiria, "Loo, vema, mnajua, hiyo ni namna fulani ya ninii . . ." kama tu walivyomfanyia Yesu. Walisema, "Vema, yeye ni Beelzebuli, yeye ni mpiga ramli, ibilisi." Beelzebuli alikuwa roho ya ibilisi. Walisema alikuwa akifanya hiyo kama mpiga ramli, Beelzebuli. Na mtu yeyote anajua kwamba upiga ramli ni ibilisi. Hakika ndivyo. Wowote wa mikutano hiyo ya kuwasiliana na mizimu, na uchawi, na kadhalika, ni ibilisi. Hakika ndivyo. Ni ibilisi akijaribu kumwiga Kristo. Kwa sababu kuna ibilisi, hiyo inaonyesha kuna Kristo; maadamu ubaya upo, kuna wema unaotokana nao. Amina. Maadamu tuna mpiga ramli, inaonyesha tuna nabii halisi mahali fulani. Hiyo ni kweli. Loo, jinsi ninavyomshukuru Mungu kwa wema Wake!

227 "Yachunguzeni Maandiko; ndani Yake mnadhani mna Uzima wa Milele, Nayo yananishuhudia Mimi." Sikilizeni yale, tena, aliyosema, "Nisipozitenda kazi za Baba Yangu, kama kazi Zangu hazitoi hiyo Sauti dhahiri ya Injili, basi msiamini." Whiu! Yeye alikuwa . . . Hakuna shaka kuhusu hilo. "Nisipoyatenda mambo ambayo Mungu alisema ningefanya, basi msiniamini Mimi." Hakuna shaka kuhusu hilo.

228 "Mnadai kuwa ninyi ni kundi la Kimaandiko," Akasema, "basi nisipoyatenda mambo ambayo Mungu alisema kwamba . . . kwamba nitayatenda, basi msiniamini Mimi. Endapo Maandiko hayajishuhudii Yenyewe kupitia Kwangu, vema, basi msiniamini Mimi." Loo, hakuna shaka kuhusu hilo. La, hasha. "Nisipozifanya kazi hizo, basi msiniamini Mimi. Lakini nikizitenda hizo kazi, basi niaminini Mimi." Hakuna, hakika, hakuna sauti isiyojulikana, tena, kuhusu hilo.

229 Na tena, alisema hivi, sikilizeni sasa: "Ninao uwezo wa kuutoa uhai Wangu, na ninao uwezo wa kuutwaa tena." Amina. Hakuna shaka kuhusu hilo, sivyo? Ninayaruka Maandiko mengi kwa sababu ya kuchelewa. "Ninao uwezo wa kuutoa uhai Wangu, ninao uwezo wa kuutwaa tena."

230 Sikilizeni, Yesu alisema, Biblia, Kristo, katika Yohana 14:12, "Aniaminiye Mimi," si anayejifanyaya kuamini, lakini "yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi yeye naye atazifanya." "Atazifanya!" Sio, "Labda atazifanya"; "Anapaswa kuzifanya." "A*ta*zifanya." Hakuna shaka, kuhusu hilo, alisema, "Watazifanya."

231 Yeye alifanya kazi za aina gani? Alionyesha kazi za aina gani? Aliitwa nani? Ibilisi kwa kufanya hivyo. "Ikiwa wanamwita Bwana wa nyumba Beelzebuli, je, si zaidi sana watawaita wale walio wanafunzi Wake?" Hakuna shaka, alisema, "Kama—kama . . . Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi yeye naye atazifanya." Hakuna shaka.

232 Tena, Yeye alisema, katika Yohana Mtakatifu, "Mkikaa ndani Yangu, na Neno Langu likae ndani yenu, basi ombeni mtakalo," loo, "nanyi mtatendewa." Hakuna *mashaka*, "Mtapewa. Itafanyika." Hakuna shaka. Loo, na tutambae tutoke kwenye ganda hilo la kobe!

Ndugu, wanaume wa Mungu, wanawake wa Mungu, tuna shida gani? Kuna kitu kinachopaswa kutusogeza, *tunayumba-yumba*.

233 Nilipokuwa mvulana mdogo (Mnajua kasa ni nini, kobe? Tunao huko nyuma mashariki, maskini kobe, ndivyo tunavyowaita.) nami na ndugu yangu tulimwona mmoja, siku moja, tulikuwa jamaa wadogo, na alikuwa ndiye kitu cha kuchekesha sana ulichopata kuona, alikuwa akijongea namna *hiyo*. Basi tulipomfikia, alifanya *swoosh*, akajikunja. Inanikumbusha tu baadhi ya watu, kuwahubiria Injili, ukianza kuieneza Injili, nao *swoosh*! "Siku za miujiza zimepita. Hakuna kitu kama hicho." Maskini kasa!

234 Mnajua nini? Nikasema, "Nitamfanya atembee." Nikaenda kule na kujiokotea kiboko na kuanza kumcharaza; hiyo haikufaa kitu. Nikamcharaza tu, alijificha tu. Unaweza kuwapiga, uwacharaze, ufanye chochote utakacho, haitafaa kitu. Nikasema, "Nitamwadhibu." Nikamshusha kwenye kijito, nami nikambatiza, nikamzamisha majini, mpaka mapovu yakabubujika tu, na hakukuwa na lingine kwake. Maji hayatafaa kitu, afadhali uachane na kuzozana kwako. Nilimshikilia tu pale mpaka mapovu yote yakawa ni *povu*, *povu*, *povu* tu, wala hakufanya lolote.

235 Lakini mnajua nilichofanya? Niliokota kipande cha karatasi na kujiwashia moto kidogo, kisha nikamlaza maskini huyo jamaa juu yake, ndipo akatembea. Hilo ndilo tunalohitaji usiku wa leo, ni ubatizo wa Roho Mtakatifu na Moto, wala sana sana si kanuni za imani zinazounga mkono jambo hilo. Huko nyuma kama babu zetu walivyokuwa nayo, tunahitaji Pentekoste nyingine ambayo itawaweka sawa na Roho Mtakatifu, itakayowafanya watu kupiga magoti, kuwarejesha watu kwenye Biblia zao, kuyachunguza Maandiko na kuyatafuta.

236 Haitoi sauti isiyojulikana, inatoa yale hasa Biblia ilisema ingefanya, yale Yesu aliyosema ingefanya, "Mkikaa ndani Yangu, na Maneno Yangu ndani yenu, basi ombeni mtakalo." Kwa nini? Uko ndani ya Kristo kwa imani, nalo Neno liko ndani yako, huyo ni Roho Mtakatifu ndani yako, na ni Neno, ndipo Neno *hili* lililochapishwa linajidhihirisha Lenyewe, linalihuisha. Hakika.

237 Marko 16, baada ya kifo, kuzikwa, na kufufuka Kwake, alikuwa akiliagiza Kanisa Lake, alisema, "Enendeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe.

Aaminiye na kubatizwa ataokoka; asiyeamini atahukumiwa. Na ishara hizi zitafuatana na hao waaminio."

238 Hapana shaka. Sio, "Labda zitafuatana nao"; "Zinapaswa." "Zi*ta*fuatana na hao waaminio." Sio, "Watapeana mikono na mhubiri, na kula ule mkate mwembamba mara moja moja, na kutoa ulimi wao, naye kasisi anywe divai." Kamwe hakusema neno kuhusu hilo. Ilisema, "Ishara hizi zitafuatana . . . "

239 Loo, "Watalipa madeni yao, na kutoa zaka zao kanisani, nao ni watu wazuri, waliofanikiwa," kamwe hakusema hivyo. Alisema, "Ishara hizi zitafuatana," (Zitafuatana!) "zitafuatana na hao waaminio; kwa Jina Langu watatoa pepo; watanena kwa lugha mpya; wakishika nyoka; au kunywa vitu vya kufisha, havitawadhuru; wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya." Amina. Hakuna shaka hapo. Ilikuwa ni kweli.

240 Nabii wa Biblia anatuambia ya kwamba itakuwa Nuru wakati wa jioni. Biblia inatabiri kwamba kutakuwa na Mwana wa . . . Mungu akiangaza katika siku za mwisho wakati wa jioni, kama tu ilivyoangaza wakati wa kwanza, Kanisa la Biblia, Injili ya Biblia kama tu ilivyokuwa; itakuwa.

241 Yesu alisema, katika Maandiko, "Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, ambapo watu wanane waliokolewa . . . Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, ndivyo *itakavyokuwa* . . . " Si, "Labda, nadhani . . . " Si . . . Sasa shikilieni tu hilo kwa muda kidogo, nitaliacha likolee. "Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, watu wanane waliokolewa, ndivyo *itakavyokuwa* katika kuja kwake Mwana wa Adamu. Maana mlango ni mwembamba, na njia imesonga, lakini ni wachache watakaoipata." Ee Mungu! Tu—tu—tujalie tu tuwe hao wachache.

242 Tutafanya nini? Je, utakuwa kijazio, au utakuwa Kitu chenyewe? Kuna njia moja tu ya kufanya: Unafanyika Neno, nalo Neno linafanyika wewe; Mungu ndani yako, wewe ukikaa ndani ya Mungu, na Mungu ndani yako.

243 Tena, Yesu aliahidi, katika siku za mwisho, kwamba itakuwa hivyo, kwamba Mataifa, katika wakati wa mwisho, watapokea ishara ile ile waliyoipokea kule Sodoma, kabla ya kuteketezwa kwake. Sasa, angalieni kwenye Pwani hii ya Magharibi ambako dhambi imekuja kwa mawimbi, inaingia *hivi*, sikuzote inatoka mashariki.

244 Wakati Mhindi alipoishi hapa . . . Mtu fulani . . . Nilikuwa nikizungumza na mmishenari mmoja huko nje muda mfupi uliopita, ama mahali fulani, nilifikiri ningemwona tena, nilikuwa nikizungumza naye, mmishenari kwa Wahindi. Wakati walipoishi hapa palikuwa na amani. Kitu pekee walichokuwa nacho kilikuwa ni vita vidogo vya kikabila, hakuna utovu wa uadilifu miongoni mwao. Mzungu alipoingia, aliingia na ulevi, na wanawake, na utovu wa uadilifu.

245 Na inatoka mashariki, ikilundikana hadi magharibi. Haiwezi kwenda mbele zaidi, kuna kizuizi cha sauti papa *hapa* Mungu anacho. Wakati mashariki na magharibi zinapokutana, zinaingia, zikiisumbua Pwani hii ya Magharibi na kuning'inia, kuning'inia, kufilisika. Na kila wakati yanakuja namna hiyo, yanaanza kuwa mabaya zaidi na zaidi, kama siku za Kilutheri, kisha zikaja siku za Kimethodisti, kisha zikaja siku za Kibatisti, halafu Church of God, halafu Nazarayo, kisha Pentekoste.

246 Kila wakati adui anapoingia kama mafuriko, Roho wa Mungu huinua kiwango dhidi yake. Hayo yote, mpaka tuko kwenye wakati wa mwisho sasa, ile ishara ya mwisho ambayo Yeye alitoa. Tumekuwa na uponyaji, na miujiza, na kunena kwa lugha, na kutoa pepo, na kadhalika, hapo awali, lakini sisi hapa.

247 Kama vile Malaika yule alivyoketi huku mgongo Wake umeelekea kwenye hema, alimokuwa ndani, mle ndani, na kuelezea kile hasa alichokuwa akisema pale, Yesu alisema, "Ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu." Itakuwa hivyo. Israeli waliipokea huko, Mataifa, Wayahudi, Wasamaria, na sasa Mataifa. Itakuwa hivyo. Kwa nini? Biblia ilisema, "Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo na hata milele."

248 Hakuna shaka juu yake. Yeye ni yule yule. Naye anapokuja katika utimilifu Wake katika siku hizi za mwisho, akijidhihirisha Mwenyewe, anajithibitisha Mwenyewe yeye yule. Amina. "Sifanyi neno ila Baba anionyeshe kwanza." Loo, jinsi ninavyotamani ningeweza tu kuwafanya watu walione! Mnaona? Laiti ningaliweza. Sawa.

249 Hakuna shaka. "Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo na hata milele." Waebrania 13:8. Hiyo ni kweli? Bila shaka ni kweli. Mnasema, "Vema, Ndugu Branham, sijui la kufanya." Biblia ilisema katika Matendo 2:38, "Tubuni kila mmoja wenu, mkabatizwe katika Jina la Yesu Kristo kwa ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea Kipawa cha Roho Mtakatifu." Si, "Huenda mkapokea." "Mtapokea!" Hakuna shaka kuhusu hilo, hakuna shaka hata kidogo.

250 Akasema, "Mtampokea. Kwa maana ahadi hii ni kwa ajili yenu na kwa watoto wenu, na kwa wote walio mbali, na wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie." Aliahidi kufanya hivyo. Hapo hapana shaka. Mtampokea, hakuna tashwishi.

251 Maskini Zakayo katika Biblia, mke wake, Rebekah, alikuwa m—mfuasi wa Bwana Yesu. Ushawishi wake ndio uliosaidia kumleta pale, tunaambiwa na historia. Anataka . . . Alitaka Zakayo amwamini Yesu sana, kwamba Yeye alikuwa nabii. Naye akamwambia, kamwambia, kasema, "Mpenzi, Yeye . . . Mtu huyo ni nabii, ninamwona akisimama pale na kusema kile ambacho mtu huyo alitambua moyoni mwao. Sasa, angalieni hapa, Maandiko yanasema . . . Hili hapa thibitisho kamili kwamba Yeye . . . "

252 “Aw, Rabi Kabinski,” natumai hakuna mtu kama huyo hapa, lakini, “Rabi Kabinski aliniambia kuwa haikuwa kitu ila lundo la udanganyifu. Nini kinachomfuata? Kundi la baradhuli ambao hawakuwahi kwenda shuleni hata siku moja maishani mwao.” Ibilisi huyo wa kale kamwe hakufa. Hakika. Hivyo akasema, “Hao ni akina nani? Siamini.”

253 Lakini mnajua, alimwombea mara kwa mara. Na wakati ile siku alipokuja mjini, alifikiri angekutana Naye, aone jinsi alivyokuwa. Hakuamini Yeye alikuwa nabii, kwa hiyo akasema, “Nitamdanganya tu. Nitapanda juu ya mti, na kumwangalia anapopita.” Naye akajifunika, akapanda juu ya mti.

254 Huyu hapa Yesu anakuja akitembea barabarani, akitembea namna *hii*. Alikuja moja kwa moja chini ya mti, akatazama juu kwenye mti, na kusema, “Zakayo, shuka chini.” Hakuna shaka kuhusu hilo.

255 Zakayo akasema, “Naam, Bwana, mimi hapa. Ikiwa nimefanya jambo lolote baya, nitalirekebisha.” Alijua alikuwa nani, pia alijua alikuwa hapo juu ya mti huo pia.

256 “Zakayo, shuka chini; ninaenda nyumbani nawe kwa chakula cha jioni.” Akayaachilia hayo matawi, naye huyu hapa anakuja. Alijua Huyo alikuwa ndiye Masihi. Hakukuwako na sauti isiyojulikana hapo. Alijua Ndiye.

257 Lakini, siku hizi, jambo lilo hilo linaweza kutokea, waseme, “Loo, vema, ulikuwa ni mkutano mzuri sana, nadhani.” Loo, jamani! Injili hii isiyoghoshiwa ikihubiriwa kwa kizazi kilichopotoka, ni jambo la kuhuzunisha sana. Lakini hata hivyo, neema ya Mungu inalishurutisha kuendelea hata hivyo, “hataki mtu yeyote apotee, bali kwamba wote waifikilie toba.” Naam.

258 Sio tu kwamba alijua alikuwa kwenye mti, bali alijua yeye alikuwa ni nani, “Shuka chini.” Hilo liliondoa kabisa ugumu kutoka ndani yake. Mnajua, akawa mshiriki kamili wa Shirika la Wafanyabiashara wa Full Gospel huko chini, naamini, huko chini . . . huko chini. Mbona hakika. Alishawishika ya kwamba Huyo alikuwa ndiye Masihi. Haidhuru Rebekah alifanya nini, ama Rebekah alisema nini, alijionea mwenyewe. Naam, bwana.

259 Nathanaeli, yule mwanachuoni aliyefunzwa vyema tuliyekuwa tukizungumza habari zake hivi majuzi usiku, alipokwenda pale, alisema, “Nitaenda nijionee.”

Basi alipokuja, Yeye alisema, “Tazama, Mwi—Mwisraeli kwelikweli, ambaye hamna hila ndani yake!”

Kasema, “Ulinijua lini Wewe, Rabi?”

Akasema, “Kabla Filipo hajakuita, ulipokuwa chini ya mti, nalikuona.”

260 “Wewe ndiwe Mfalme wa Israeli; Wewe ni Mwana wa Mungu.” Hakuna shaka hapo. Alijua kabisa alikuwa chini ya mti. Loo, naam. Kamwe hakusema, “Mbona, hao Mafarisayo

walisema huyo ni Beelzebuli!" Lakini si Zakayo. Alijua ndiye aliyekuwa chini ya mti. Hakuna sauti isiyojulikana kwa Zakayo. Jina lake lingali hai usiku wa leo, na litakuwa daima kwa sababu aliokoka.

261 Maskini mwanamke yule kisimani, alikuwa ameona aibu nyingi kuhusu dini zao zote, nayo makanisa, na—na theolojia ya siku hiyo mpaka akawa mgonjwa na amechoshwa na hayo yote, hakuhudhuria hata moja ya hayo. Sijui, alikuwa bora bila hayo. Maskini huyo mtoto labda, kwa wazazi wabaya, aliachiliwa huko nje mitaani, ndipo akawa kahaba. Labda maskini huyo jamaa hakuwa na . . .

262 Acheni niwaambie, kuna wanawake wengi wabaya, tunajua hivyo, lakini huwezi kuwa mwanamke mbaya bila, kuwapo na mwanamume mbaya, mwajua. Kwa hiyo inabidi kuwe na mtu wa kumharibu. Kwa hiyo, na wakati mwingine hao watoto hufukuzwa na mama mbaya, anayekimbilia vyumba vya baa na kadhalika.

263 Mnazungumza juu ya kutowajibika kwa watoto, mimi nasema ni kutowajibika kwa wazazi. Mnazungumza juu ya ujinga wa Wakentaki, baadhi ya maskini akina mama hao huko nje, acha binti zao warudi nyumbani asubuhi moja wamejipaka rangi ya midomo kote usoni mwao, na nywele zimesokotwa kabisa, na nusu uchi, nguo zimechafuka nusu, wakiwa na sigara mkononi mwao, wangeokota kipande cha ubao mwembamba, ama mojawapo ya vijiti vya hikori huko nje, naye angejua alipotoka wakati mwingine! Kisha mnasema, "Hawana elimu." Wanaweza kulifundisha kundi hili la majambazi wa kutisha jinsi ya kulea watoto. Hiyo ni . . . Loo, vema, labda sikupaswa kusema hivyo. Vema, la, silighairi, nilisema hivyo wakati Roho Mtakatifu alipokuwa akinitia mafuta. Hiyo ni kweli, kweli kabisa. Naam, bwana. Leo, hmm! Loo, jamani.

264 Maskini mwanamke huyo, alizurura huko kisimani asubuhi hiyo, labda misokoto yake ya nywele yote ikining'inia chini, labda alikuwa nje usiku kucha, sijui mimi. Alitoka yapata saa tano kuchota maji ya siku hiyo, ndipo alipotazama kule na kumwona Myahudi huyo, Myahudi huyo alisema, "Nenda kamwite mumeo."

Akasema, "Sina yeyote."

Kasema, "Unasema kweli. Unao watano; naye unayeishi naye siye wako." Masalale!

265 Kasema, "Bwana," hakuna sauti isiyojulikana, hakuna shaka kulihusu, "Naona ya kuwa Wewe ni nabii. Sasa, najua ya kwamba ajapo Masihi, na sisi sote hapa chini Sikari tumefundishwa, sisi Wasamaria, kwamba ajapo Masihi atafanya hivi. Ninashangaa u Nani Wewe."

Yesu akasema, "Mimi Ndiye." Hakuna sauti isiyojulikana, akasema, "Mimi Ndiye."

Mtu fulani akasema kamwe Yeye hakukiri kuwa Mwana wa Mungu. Vipi kuhusu hilo? Kasema, "Mimi ninayesema nawe Ndiye."

266 Tazama. Ndugu, hakusema, sasa, "Je, niende shule na kujifunza theolojia kidogo?" Alikimbilia mjini na kusema, "Njoni, mwone Mtu, aliyeniambia mambo ambayo nimefanya. Haimkini Huyo kuwa ndiye Masihi?" Hakuna shaka hapo. La, bwana, alijua. Akasema, "Tumefundishwa ajapo Masihi, hivyo ndivyo atakavyofanya."

267 Sasa, marabi walifikiri ilimbidi kufanya *hivi na hivi*, dhehebu *hili* lilifikiri *hivyo*, nalo *hili* lilifanya lipendavyo, nao wote walikuwa wametengana na kadhalika, na wote wamekauka, na kuelimika vilivyo, na kujivuna, na loo, kama vile baadhi ya wanawake hawa wanavyojaribu kujinyoosha katika nguo hizi za kisasa kama soseji iliyotolewa ngozi, ama kwa namna fulani kama, kwenda chini namna hiyo, akiingia na kutoka, na kutoka na kutoka. Sisemi hivyo kwa mzaha. Hapa si mahali pa mzaha, hapa ni mahali pa kufanya ukweli, kweli. Hiyo ni kweli. Ni aibu na fedheha.

268 Wala hiyo si fedheha kuliko watu wanaojaribu kuchukua aina fulani ya fundisho la sharti na kulishindilia chini kwenye shingo ya mtu. Kama ungeenda kwenye mkahawa na kuchukua bakuli la supu, nalo lilikuwa na buibui ndani yake, ungeushtaki huo mkahawa, lakini mnaruhusu baadhi ya nyumba hizi za maiti humu ndani ambao kipimajoto chao kinaonyesha elfu moja chini ya hali ya kawaida, na kuwadunga baadhi ya hiyo dawa ya kuzuia maiti isioze waliyo nayo mle, wakati wewe . . . wakuweke umekufa siku zote za maisha yako, halafu usiseme lolote juu yake, wakati mwili huo hauna budi kufa kwa vyovyote vile, bali nafsi hiyo huishi milele mahali fulani. Kuna nini? Kuna sauti isiyojulikana kwake.

269 Yesu alisema, "Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi, yeye naye atazifanya." Hakuna shaka hapo. "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio." Hiyo ni kweli. "Yeye aniaminiye Mimi, ajapokufa, hata hivyo atakuwa anaishi. Na yeye aishiye na kuniamini Mimi hatakufa kamwe." Hakuna shaka kuhusu hilo. Ufufuo ni hakika. Kweli.

270 "Aulaye mwili Wangu, na kuinywa Damu Yangu, yuna Uzima wa Milele; nami nitamfufua siku ya mwisho." "Bali yeye alaye na kunywa isivyostahili, hula na kunywa hukumu, kwa kutokuupambanua Mwili wa Bwana." Hakuna shaka juu ya lolote la hilo. Hiyo ni kweli. Ukila inavyostahili, ukitembea katika Neno, katika imani, Mungu aliahidi ufufuo. Ukila isivyostahili, umekufa wakati uo huo unapoishi. Biblia ilisema mwanamke aishiye katika anasa amekufa angali hai. Kweli kabisa. Biblia ilisema hivyo. Hilo ni Neno la Mungu lisilo na

kikomo, haliwezi kubadilika. Bila shaka. Loo, hakuna sauti isiyojulikana!

271 Hapa si muda mrefu uliopita, nilikuwa huko chini Meksiko. Nafunga. Tulikuwa na mkutano mzuri sana. Jemadari Medina, wengi wenu mnamjua, yule jemadari mkuu wa Meksiko, alimwendea gavana, akapata kibali cha mimi kuingia. Naye askofu huko Rumi, uh, askofu wa Kirumi, askofu wa Katoliki, akamwendea na kusema, "Bwana, huyu mtu anayekuja, si Mkatoliki." Akasema, "Serikali yetu haipaswi kuruhusu mambo kama hayo."

272 "Loo," askofu akasema, "Jenerali Medina anamleta. Nafikiri ni mtu mwenye sifa nzuri. Yeye . . . Wanasema ana umati mkubwa wa watu," na kadhalika.

"Loo," akasema, "hakuna kitu kinachotoka kwenda kusikia mambo hayo, kama hayo, ila wajinga na wasio na elimu."

273 Serika- . . . Rais akamwambia, akasema, "Bwana, mmekuwa nao kwa miaka mia tano, kwa nini wao ni wajinga na wasio na elimu?" Kasema, "Nijuavyo mimi, anaweza kuja."

274 Loo, jamani! Ningeweza kutembea huko, kasema, "Uh-huh." Nikaenda mle, nikaingia mle ndani, na kuwa na mkutano. Hao Wameksiko maskini! Takriban siku tatu tu usiku ndizo tu tulizokuwa na nafasi ya kuweka stendi, ambapo maelfu mara maelfu . . .

275 Ni wangapi wanaomjua Ndugu Espinoza, mfasi- wa Kimeksiko . . . huku chini, yule ndugu, huku chini, California? Alikuwa mkalimani wangu. Nimeona baadhi ya mikono yenu ikiinuliwa. Alikuwa akinifasiria.

276 Usiku huo, wakija jukwaani, hawakuwa wamewahi kuona kitu kama hicho. Hapo walisimama wote, hakuna mahali pa kuketi. Walikaa hapo saa tatu asubuhi hadi saa tatu usiku huo, wakati ningefika pale, wakiegemeana, wakiwalundika wagonjwa wao kwenye malundo namna *hiyo* (Acheni Ndugu Espinoza awaonyeshe hizo picha.), na magari yaliyojaa viti vya magurudumu na machela.

277 Mzee mmoja wa Kimeksiko alipitia jukwaani usiku huo mmoja, naye alikuwa akienda . . . alikuwa kipofu. Alikuwa na kofia kuukuu iliyoshonwa kwa kamba, hana viatu miguuni, kama mguu wa dubu chini, miguu ya suruali juu kabisa, imechanika, amevaa koti kuukuu lililochakaa, amejaa mavumbi, akija juu kipofu. Akaingiza mkono ndani ya maskini mfuko huo mchakavu na kutoa msalaba mdogo, alitaka kukariri "Salamu, Maria," Nilimwambia kwa Ndugu Espinoza, "Weka kitu hicho mfukoni mwako," ndipo akaja pale.

278 Nami nikamwangalia maskini huyo mzee, nikawaza, "Jamani!" Kipofu kabisa, nikawaza, "Kama baba yangu angeishi, angekuwa karibu umri huo." Mimi huyu hapa nimevaa

suti nzuri, jozi nzuri ya viatu, na hapo alisimama mzee yule akiwa hana kitu. Nikawazia, "Labda hajawahi kupata mlo mzuri maishani mwake, nami hula vizuri."

279 Nikaweka mguu wangu kando ya wake, nione kama viatu vyangu vingemtosha, niliwazia ningeweza kuvitoa, kusanyiko lisingeweza kuona. Nikaweka mabega yangu kando ya yake, nione kama mabega yangu yataenea—lingemwenea, koti langu. Bila shaka, alikuwa mkubwa zaidi, na miguu yake ilikuwa mikubwa zaidi, basi nisingeweza. "Ee Mungu, angalia hapo." Kabla hujaweza kuwaombea watu, huna budi kuhisi ha—hali zao. Huna budi kuwahurumia.

280 Hilo ndilo siwezi kuelewa siku hizi, madhehebu yetu yakijipanua, na kujenga mamilioni ya dola za majengo, kisha kuhubiri kuja kwa Bwana kumekaribia, na maskini wamishenari huko ng'ambo ambao hata hawana viatu miguuni mwao, wakiibeba Injili hii ya Yesu Kristo.

281 Walipotoa sadaka kule, maskini mwanamke mkongwe alijitokeza, hana kitu ila maskini jozi ya makubadhi tu, akayatoa kama sadaka, aliwazia mwanamke mwingine anaweza kuzitumia vizuri zaidi kuliko yeye. Na usiku wa leo, sisi pamoja na ninii yetu nyingi . . . Ee, Mungu, usiniruhusu nianze jambo hilo. Naam, bwana. Tunawezaje kuweka mamilioni ya dola (Tuseme, "Naam, wao si wa kundi letu." Mungu na aturehemu, mtu anapoondoa mawazo yake kwenye kundi. *Huko* ndiko tunakozungumzia, *Huko* juu! Tusimame kwenye Neno hili!), wakati hao watu maskini hata hawajui mkono wa kuume na wa kushoto ni upi, nao wanataka kumjua Kristo?

282 Hao hapo Wameksiko maskini wamesimama pale, wameegemeana. Nikamwangalia huyo jamaa mzee, nikawaza, "Mungu, uturehemu." Najua jambo moja tu ninaloweza kufanya, siwezi kuzungumza lugha yake, nikamvuta tu karibu nami, nikasema, "Baba wa Mbinguni, ninamwombea maskini huyu mzee." Hawafasiri maombi. Nikasema, "Ninamwombea." Nikasema, "Tafadhali . . . "

283 Ndipo nikafungua macho yangu, naye huyo hapo amesimama mbele yangu, akiniangalia. Hakuna shaka kuhusu hilo, Ndugu. La, la. Mara nikamsikia akipaza sauti, "Gloria a Dios!" Inamaanisha "Utukufu kwa Mungu." Huyo hapo, angeweza kuona vizuri kadiri nilivyoweza. Huyo akipanda huku na huko kupitia pale, akipaza sauti na kumsifu Mungu.

284 Basi kesho yake usiku, kulikuweko, kama mara tatu ama nne kwenye jukwaa hili, kulikuwa na malundo ya shela kuukuu na makoti chakavu yamelundikana juu *hivi* yapate kuombewa. Hapa wangeweza . . . Ilibidi wanishushe chini juu ya uwanja huo mkubwa wa michezo ya ng'ombe, huku nimefungiwa kamba *hivi*, nipate kufika mahali walipokuwa hao watu. Nami nikashuka kule, na ilikuwa . . . ilikuwa ikinyesha siku nzima, nao

hao hapo wamesimama, wamelala, wamelundikana mmoja juu ya mwingine, na kadhalika, mchana kutwa.

285 Basi kulikuwa na mwanamke mdogo pale usiku huo, maskini mwanamke Mkatoliki, usiku uliotangulia, alikuwa na mtoto mgonjwa, asingeweza kufika mahali ilipokuwa. Basi kesho yake asubuhi alimpeleka mtoto wake kwa daktari, akafa, moja kwa moja katika ofisi ya daktari saa tatu kwa nimonia, nao wakamleta huyo mtoto mchanga. Alikuwa . . . akarudi kule, yapata saa nne na nusu. Akasimama pale kwenye mvua hiyo mchana kutwa, ndipo wakati ndugu aliposambaza kadi za maombi . . . Ndugu fulani, nilimwita "Mañana," kwa sababu alikuwa mwenda pole sana. Kamwe hakufanya lolote. Nami . . . Alikuja, alipaswa kunichukua saa moja, naye alinichukua yapata saa tatu. Nikasema, "Mañana"; maana yake "kesho," mwajua. Kwa hiyo alikuwa akisambaza kadi za maombi. Basi akasambaza kadi zake za maombi, naye huyu mwanamke hakupata.

286 Waliponishusha kwenye huo uwanja, nilitoka pale na, jukwaani, nikaanza kuzungumza: *Imani Ni Kuwa Na Hakika Ya Mambo Yatarajiwayo*, Nikasema, "Sasa, Yesu Kristo, katika Biblia, wengi wenu ninyi watu mmeisoma Biblia," huku Ndugu Espinoza akifasiri, nikasema, "kile alichokuwa Yeye, hana budi kubakia vile vile. Alichokuwa . . . Alisema hakufanya neno mpaka Baba alipomwonyesha. Lolote ambalo Baba alimwonyesha, hilo alilifanya. Kwa maneno mengine, aliigiza katika mchezo wa kuigiza. Ni hakika." Na wakati niliposema hivyo, nikasema, "Hiyo ni imani Yake, kwa maana Baba alikuwa amemwonyesha, Yeye alijua la kufanya hasa."

Na yapata wakati huo Billy akaja, akanivuta koti, akasema, "Baba, itabidi ufanye jambo."

Nikasema, "Kwani kuna nini?"

287 Kasema, "Nina mabawabu mia sita wamesimama *pale* chini, na kuna mwanamke mdogo mwenye mtoto mchanga aliyekufa mikononi mwake, naye atapanda juu ya mgongo wao, na kukimbia katikati ya miguu yao. Naye hana kadi ya maombi, nasi . . . hakuna mabawabu wa kutosha" mia sita, "kumwondosha kwenye jukwaa."

288 Ndugu, alikuwa ameyakinia. Hiyo ni kweli. Aling'ang'ania. Kweli alikusudia kufika huko, hivyo tu. Aliamini, kulikuwa kuna Sauti iliyomgusa, wala haikuwa isiyojulikana. Alijua kama Mungu aliwahi kuwa Mungu, Yeye alikuwa ni Mungu hata leo.

289 Nikamwambia Ndugu Jack Moore, wengi wenu mnamfahamu, wa Shreveport, nami nikasema, "Ndugu Jack, yeye hanijui, nenda kule, na ushuke upitie kwenye hao mabawabu, na kumwombea huyo mtoto. Yeye hatajua tofauti, endelea."

Akasema, "Vema, Ndugu Branham." Akaanza kuondoka.

Naye Ndugu Espinoza akasema, "Niseme nini?"

290 "Endelea tu na kusema kama nilivyosema." Nikasema, "Kama nilivyokuwa nikisema, Yesu alisema alifanya . . ." Nikaangalia, amesimama mbele yangu, papo hapo kivulini, moja kwa moja mbele yangu kulikuwa na maskini mtoto mchanga wa Kimeksiko, asiye na meno, fizi zake ndogo tu, akitabasamu nami. Loo, Ndugu, hakuna shaka kuhusu hilo! Nikasema, "Ngoja kidogo, Ndugu Jack, mwambie amlete huyo mtoto hapa."

291 Mabawabu wakarudi nyuma, ndipo maskini mwanamke huyu mdogo, mwenye sura ya kuvutia akaja pale mbio, akapiga magoti akaanza kupiga mayowe, "Padre! Padre!" Maana yake "Baba."

Nami nikasema, "Simama."

292 Naye Ndugu Espinoza akamwambia, "Simama." Naye, huku amemshika mtoto huyu mchanga, blanketi juu yake, umbo dogo lilioshupaa limelowa maji kabisa, amesimama pale tangu saa nne asubuhi hiyo, ilikuwa karibu wakati huu usiku. Aliingia pale yapata saa nne.

293 Nami nikasema, "Ndugu Espinoza, usifasiri hili. Nimeona ono hivi punde, sijui linamaanisha nini. Nilimwona maskini mtoto huyo mchanga, alionekana kama yeye, amesimama papa hapa." Nikaweka mikono yangu juu ya umbo hilo dogo baridi, nikasema, "Baba wa Mbinguni, sijui hii inamaanisha nini, lakini Wewe ulinena. Nami nilikuwa tu nikisema ulisema hukufanya neno mpaka Baba alipokuonyesha. Mtoto huyo mchanga alimaanisha nini alipokuwa akitabasamu mbele yangu?"

294 Yapata wakati huo huyo mtoto mchanga akafanya, "Whaah, whaah, whaah." Hakuna sauti isiyojulikana. Jamani, kila mtu akaanza kupiga mayowe na kuanguka. Wakanizungushia kamba, wakaninyanyua kutoka kwenye huo uwanja tena, wapate kuniondoa kwenye mauaji yanayokuja tuseme, watu wakija mbio walivyoweza kuja.

295 Nikasema, "Ndugu Espinoza, usilitangaze hilo. Kwanza, kila kitu tunachochapisha hakina budi kuthibitishwa." Naam, bwana. Nikasema, "Sijui kile huyu mwanamke . . . Nilimwona tu mtoto mchanga."

296 Naye akamtuma mtu fulani pamoja na huyo mwanamke, ndipo kesho yake asubuhi akaja nayo, akamwendea huyo daktari, naye daktari akasaini taarifa. Ilikuwa katika *Sauti* ya Wafanyabiashara wa Full Gospel. Mambo hayo yanapochapishwa, itabidi kuwe na kitu cha kuyaunga mkono. Na huyo hapo daktari aliyeisaini, "Nilitangaza mapigo ya moyo ya mtoto huyo kuwa yamekoma, amekufa, asubuhi hiyo saa tatu. Na kesho yake asubuhi alikuwa ofisini mwangu, yu hai kabisa." Ni nini? Hiyo si sauti isiyojulikana. Hiyo ina maana kwamba

Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Haleluya! Mnaamini?

297 Hebu tuinamishe vichwa vyetu basi. Siwezi tu kuendelea, nitarudi wakati mwingine kuwaletea Maandiko haya mengine. Mnaamini? "Baragumu ikitoa sauti isiyojulikana, ni nani atakayejiweka tayari kwa vita?"

298 Loo, kuna vita vinavyokuja kwa kila mmoja wenu, na hivyo ni vita vya mauti, huna budi kuvikabili. Mnakumbuka jana usiku? Lakini kulikuwa na Shujaa mmoja mkuu aliyekutangulia na kuuchomoa huo mwiba kwa ajili yako. Alifufuka katika wafu, Yu hai hata milele. Si sauti isiyojulikana, yu hai milele, Yeye yuko papa hapa sasa. Yeye hashindwi, Yeye ni Kristo. Je, mnamwamini? Aminini tu.

299 Ni wangapi hapa ndani wasio na kadi za maombi? Nimechelewa sana kufanyiza mstari wa maombi sasa hivi, nitazichukua kesho. Wewe usiye na kadi ya maombi, inueni mikono yenu nipate kuwaona. Vema. Ni karibu tu, kwa jumla, kila mahali. Aminini.

300 Je, mnaamini ya kwamba Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele? Biblia ilisema kwamba Yesu Kristo ni Kuhani Mkuu anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu. Hiyo ni kweli? Hakuna sauti isiyojulikana hapo. Hiyo ni Biblia. Mnaamini inatoa Sauti ifaayo? Kila Neno Lake ni kweli. Haihitaji kufasiriwa kwokwote, Biblia ilisema ya kwamba ni . . . Maandiko si ya kufasiriwa apendavyo mtu yeyote, tayari yamefasiriwa jinsi tu yalivyoandikwa. Hayahitaji mafundisho yoyote ya sharti kuongezewa Kwake kuyafanya *hivi*. Yanapaswa kuwa jinsi tu yalivyo, "Yeyote atakayeondoa Neno moja kutoka Kwake, ama kuongeza moja Kwake . . . " Aminini.

301 Ikiwa ni yeye yule jana, leo, na hata milele, Kuhani Mkuu yeye yule, wewe kuwa na imani na uguse upindo wa vazi Lake, ambaye ameketi mkono wa kuume wa Ukuu wa Mungu Mbinguni, uone kama Yeye hatakujibu tena. Sasa, yale ambayo nimefundisha yatakuwa maneno ya bure kama ninii ya Mungu . . . kama Kristo alikufa wala hakufufuka tena, kama hakufufuka.

302 Unaona, ninajaribu kukwambia, rafiki, hili halijafanyika, hakuna taarifa yake, mwulize msomaji yeyote wa Biblia, mwulize yeyote—mwanahistoria yeyote, hakujawahi kuwa na taarifa ya jambo hili kufanywa katika kanisa la Kikristo, tangu kifo cha mitume, hakuna mahali popote katika historia, lakini hili hapa katika wakati wa jioni. Ni wakati wa Mataifa sasa, Mungu aliahidi jambo hilo. Je, hamwezi kuona kuwa ni Maandiko?

303 Sasa, aminini. Niangalieni. Amini kwa moyo wako wote, kwamba Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu, Naye alinituma kama mjumbe kwako. Nami sijasema maneno yangu mwenyewe,

nimesema Maneno Yake; siyaamini maneno yangu, ninaamini Maneno Yake. Kama wazo langu ni kinyume na Maneno Yake, wazo langu si sahihi.

304 Na kama Neno Lake linakaa *hapa* ndani, na ahadi aliyosema, "Kazi nizifanyazo Mimi ninyi nanyi mtazifanya," nayo Biblia ilisema Neno la Mungu lina ukali kuliko upanga ukatao kuwili, na Mtambuzi wa mawazo ya moyo, amini.

305 Ni wangapi walioona ile picha ya yule Malaika, ile Nuru? Naam, nadhani mmesikia hiyo hadithi. Meneja na hao wamewaambia kuihusu. Haiko futi mbili kutoka mahali ninaposimama sasa hivi. Hakuna sauti isiyojulikana hapo. Ni ukweli.

306 Siwezi kuponya, hakuna mtu anayeweza kuponya, hakuna daktari awezaye kuponya. Hakuna daktari atakayekwambia anaweza, dawa haiponyi, ni msaada tu. Mayo Brothers walisema, "Hatudai kuwa waponyaji, tunadai tu kuisaidia maumbile. Kuna Mponyaji mmoja, huyo ni Mungu."

307 Daktari anaweza kuweka mkono wako, lakini ni nani anayeuponya? Ni nani anayeumba hizo seli? Daktari anaweza kung'oa jino, lakini ni Nani anayeponya tundu linamotoka? Daktari anaweza kukuondolea uvimbe, lakini ni Nani aponyaye mahali hapo? kutoa ubavu, lakini ni Nani aponyaye shimo unamotoka? Mungu ndiye Mponyaji pekee. Yeye ni Muumba, na inahitaji Muumba kulitekeleza. Hawawezi kuzidisha seli, huyo ni Mungu pekee. Aminini tu.

308 Mtu fulani, asiye na kadi ya maombi sasa, ambaye hatakuwa mstarini, amini tu. Kuna mama, anayeketi papa hapa, kidogo ni mwanamke wa makamo, mkongwe, amevaa nguo ya waridi, anasumbuliwa na kikohozi cha kikoromeo. Ikiwa ataamini kwa moyo wake wote, hicho kikohozi kitamwacha. Unaamini, utakubali? Inua mkono wako, kisha useme, "Ninaukubali." Mungu akubariki.

309 Sijapata kumwona huyo mwanamke maishani mwangu. Hivi hamwezi kuiona Nuru hiyo inayoning'inia juu ya mwanamke yule pale, bado? Sasa, Hii hapa inajongea, inakuja hapa. Iweni na kicho, iweni na kicho, tafadhali. Msisogee. Mnaona, kila mmoja wenu ni roho. Na wakati ninii, upako huo unapokuja, unaposogea, unaona, i—i—inatiishwa kila roho. Mnaona? Ni wangapi wanaojua Biblia ilisema humtii nabii. . . hutii. . . ? Iweni na kicho kabisa, tulieni. Iliniacha.

310 Ni mwanaume, anayesumbuliwa na tatizo la moyo. Bw. Bailey, kama utaamini kwa moyo wako wote, Mungu atakuponya. Unalikubali? Vema, Bwana, simama kwa miguu yako na ulikubali, na tatizo lako la moyo litakuacha.

311 Huyo hapo. Simjui mtu huyo, sijawahi kumwona maishani mwangu, hatufahamiani kabisa. Lakini mtu huyo alikuwa ameketi pale, akiomba basi Bwana Yesu auguse mwili wake.

Hiyo ni kweli, Ndugu Bailey? Amini kwa moyo wako wote sasa, na litatoweka.

312 Hapa, dakika moja tu. Huyu hapa mtu mwingine anatokea, mtu fulani anaomba. Ni mwanaume aliye na ugonjwa wa tumbo. Bw. Cooper, amini kwa moyo wako wote. Ugonjwa wako wa tumbo umekuacha, Bwana. Umekuwa ukisumbuliwa na tumbo lenye fadhaa kwa muda mrefu, limekwisha sasa.

313 Simjui mtu huyo, sijawahi kumwona maishani mwangu. Mwulize upate kujua. [Ndugu fulani anasema, "Hiyo ni kweli. Ninamjua, Ndugu. Hiyo ni kweli."—Mh.] Unamjua? ["Naam."] Sawa. Hiyo ndiyo shida, na lolote alilosema ni kweli? Huyo ni mchungaji wako. Amini. Usiwe na shaka.

314 Mtu anayeketi hapa akiniangalia, ana shida ya macho yake, shida ya miguu yake. Simjui, kutoka British Columbia, Canada. Ataamini kwa moyo wake wote, yote yatamwacha. Ukitaka kuamini, sawa, Mungu atakujalia.

315 Mwanamke mdogo anayeketi hapa akiomba, ana ugonjwa wa tumbo, ana kitu kama kikoromeo cha tumbo. Sifahamiani na huyu mwanamke. Ni uvimbe, maji kwenye tezi, nadhani wanauita kikoromeo cha tumbo. Sikujui, mama. Unaonekana kuwa mwaminio. Je, hatufahamiani? Unaniamini mimi kuwa ni nabii wa Mungu? Niangalie, basi. Hutoki hapa, unatoka Idaho. Hiyo ni kweli. Jina lako ni Bibi Smith. Rudi nyumbani, kitu hicho kitakuacha, kama tu utaamini katika Jina la Yesu Kristo.

316 Unaamini? Sikilizeni, kusanyiko, siku moja kulikuwa na kijana mchungaji aliyetumwa na baba yake kuchunga kondoo. Simba akaingia na kumchukua kondoo na kumtorosha, hakuwa na mengi sana ya kumfuatilia, bali alimwamini Mungu. Alichukua kombeo dogo akatoka na kumchukua yule kondoo, naye akamrudisha, kwa sababu baba yake alimhitaji kondoo huyo.

317 Mimi ni mchungaji mdogo tu, Baba alinituma hapa. Kansa, na magonjwa, mateso yaliwashika kondoo Wake. Sina mengi sana ya kukufuata, nina maombi na imani, lakini ninakufuatilia. Ninataka kukurudisha, usiku wa leo, kwenye malisho ya kijani kibichi yenye afya njema. Naja kwenu sasa katika maombi. Mtaniamini? Wekeaneni mikono.

318 Hakuna sauti isiyojulikana. Yesu alisema, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio." Hapa juu pia, kuna magonjwa mengi sana hapa juu, nimewazuilia. Nimewazuilia, kwa sababu ninyi ni wahudumu na waimbaji. Wewe si. . . Usifikiri sijui unachofanya.

319 Wekeaneni mikono yenu. Msiwe na shaka. Kila mwaminio, usijiombee mwenyewe, omba kwa ajili ya mtu uliyemwekea mikono, anakuombea, omba jinsi ungeomba. Yesu alisema, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio. Wakiweka mikono

yao juu ya wagonjwa, watapata afya." Hakuna shaka juu yake. Hiyo ni sauti inayojulikana.

320 Baba wa Mbinguni, maskini Daudi wa kale, alijua baba aliwapenda hao kondoo, naye aliwajibika kwao, ingawa ilimbidi achukue fimbo yake, na kuwasukuma warudi mstarini, na wakati mwingine kuwapiga kidogo, lakini walikuwa kondoo wa baba. Mungu, siku moja simba aliingia na kumchukua mmoja, naye akamfuatilia, Ulikuwa pamoja naye na akamrudisha. Mungu, maradhi, magonjwa, mateso yameingia, na kuchukua baadhi ya hawa wana-kondoo, na anawatoa nje akawaue. Ninakuja Kwako, usiku wa leo, Bwana, nimewafanya wawekeane mikono, ishara ya hakika ambayo Mungu alisema itawafuata waaminio. Waliinua mikono yao walikuwa waaminio, nasi tunakuja kuwarudisha.

321 Shetani, katika Jina la Yesu Kristo, waachilie. Waache waende zao. Katika Jina la Yesu Kristo, ninaamuru ibilisi wa kutokuamini aondoke kwenye jengo hili.

322 Wekeaneni mikono. "Maombi ya imani yatamwokoa mgonjwa huyo, Mungu atawainua." Wekeaneni mikono mmoja na mwenzake, endeleeni kuomba, jifungieni ndani pamoja na Mungu. Itakuwa sawa. Loo, jifungieni ndani pamoja na Mungu, hakuna sauti isiyojulikana. Sauti hiyo inayokwambia, Sauti hiyo inayozungumza nawe ni Mungu, si sauti isiyojulikana. Ninyi Wapentekoste mnapaswa kuijua hiyo Sauti ya Roho Mtakatifu, si sauti isiyojulikana. Hizo ni nguvu Zake zinazowajia. Aminini. Mwaminini Mungu. Msitie shaka. Usitilie shaka, vunja laana hiyo ya kutokuamini ikuondokee, acha Roho Mtakatifu achukue mamlaka.

Bwana, leso hizi, katika Jina la Yesu, zipake mafuta kwa ajili ya wagonjwa na wanaoteseka.

323 Huku mmewekeana mikono, ikiwa kuna mmoja hapa ambaye hajawahi kuamini hapo kabla, ambaye anataka kukiri imani yake, usiku wa leo, katika Mwana wa Mungu Mbele za Roho Mtakatifu, ninii tu, sitakuuliza, njoo madhabahuni, simama kwa miguu yako. Simama tu kwa miguu yako, ukisema, "Ninataka kukiri imani yangu, usiku wa leo. Ilikuwa dhaifu sana, lakini sasa nimetiwa nguvu, ninamwamini kwa moyo wangu wote." Simama kwa miguu yako, mtu yeyote anayetaka kukiri hilo na kusema, "Nilikuwa siamini, lakini sasa mimi ni mwaminio." Mungu abariki. . . Ikiwa kuna yeyote kati yenu. . . Baadhi yenu simameni hapo. . . Mungu akubariki, Bwana. Mungu akubariki, Bwana. Mungu akubariki, Bwana.

324 Mtu mwingine asimame, aseme, "Nimesimama kama ushuhuda." Loo, jinsi utakavyomtaka Yeye akusimamie kwenye Siku hiyo! "Yeye atakayenishuhudia Mimi. . . " Mungu akubariki. Mtu mwingine simama kwa miguu yako, useme, "Mimi. . . Sasa imani yangu imeimarishwa." Mungu akubariki.

"Sasa, imani yangu imeimarishwa." Mungu akubariki. Simama kwa miguu yako, useme, "Sasa naamini. Ninataka kila mtu ajue ya kwamba ninaamini ya kwamba sasa hivi niko katika Uwepo wa Yesu Kristo. Niliona Neno Lake likidhihirishwa. Ninaamini tuko katika siku za mwisho. Nimesimama hapa kama shahidi. Ninamtaka Yeye awe mwema kwangu, na aondoe yote kutoka kwangu ambayo hayafanani na Yeye, na kunifanya kuwa Wake kabisa." Mungu akubariki, Bwana. Mwingine, mwingine. Njoo huku.

325 Simameni, wanaume, wanawake. Ni wangapi kati yenu watakiri hivyo, "Nimekuwa makosani, nataka kumchukua Mungu sasa"? Mungu akubariki. Mungu akubariki. Mungu akubariki. Mungu akubariki. Sasa, wahubiri na wote wamesimama. Mungu akubariki. Hapa juu, popote unapotaka kuwa, juu kwenye roshani, simama kwa miguu yako na kusema, "Sasa ninaamini, sasa ninalikubali, nimekuwa na shaka kidogo, lakini sasa ninaamini."

326 Hakuna sauti isiyojulikana. Kristo anaokoa wenye dhambi, Kristo alikufa kwa kusudi hilo. Simama. Mungu akubariki. Mungu akubariki. Mungu akubariki, wewe, loo, kundi lote, wengi wamesimama. Mungu awabariki. Mwingine? Endeleeni kusimama. "Ninaamini, ninaamini, sasa ninalikubali. Bila kivuli chochote cha shaka, sasa ninaamini katika Mwana wa Mungu. Sasa ninaamini kwamba tunaishi katika siku za mwisho. Sasa ninaamini ya kwamba niko Mbele za Yesu Kristo. Sasa ninaamini ya kwamba Neno Lake linathibitishwa, ninaliamini, ninalikubali." Simama. Mtu mwingine yeyote?

327 Baba wa Mbinguni, ninaomba dua kwa ajili yao kwa moyo wangu wote. Ninawaleta Kwako, hao ni nyara za Ujumbe. Wao ni nyara za sisi kutembelewa na Wewe, kuwa hapa usiku wa leo, kukuona ukitembea kati yetu ukifanya kazi ambayo haijawahi kufanywa tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu, mpaka siku hizi za mwisho. Hawa hapa, hao ni watoto Wako. Ninawakabidhi Kwako, Bwana. Wewe uliwakabidhi kwetu, nasi tunakukabidhi Wewe. Katika Jina la Yesu Kristo walinde na uwafufue katika siku ya mwisho.

328 Huenda nisiweze kamwe kuwasalimia kwa mkono humu duniani, lakini vita vitakapokwisha, na baragumu ya mwisho imepigwa, nao wafu wamefufuka kutoka kaburini, na walio hai wamenyakuliwa pamoja nao, ili kumlaki Bwana hewani, basi jalia nifanye ushirika na Yesu Kristo pamoja nao kukizunguka Kiti cha Enzi na kupitia nyakati za Milele zijazo. Tujalie, Bwana. Wao ni Wako. Katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

329 Wote wanaotaka kuwakaribisha katika ushirika wa Yesu Kristo, simameni kwa miguu yenu, kuwazunguka, na kuwapa mikono, usimame papo hapo karibu nao, na kuwapa mkono, useme, "Karibu, Ndugu. Karibu, Dada. Karibu, katika Ufalme

wa Mungu." Amina. Amina. Ajabu. Hilo ni jema. Mungu asifiwe. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

330 Tafuta kanisa zuri sasa, ubatizwe, na kumwita Bwana kwa ajili ya Roho Mtakatifu. Sasa, hebu sote tumwinulie Mungu mikono yetu na kuimba, "Nampenda, nampenda kwani alinipenda kwanza."

Nampenda, nampenda
Kwani alinipenda kwanza,
Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

331 Unajisikia vizuri? Sema, "Amina." Je, unajisikia kana kwamba umesuguliwa kabisa katika Uwepo wa Roho Mtakatifu hapa? Sasa, tunapouimba tena, hebu tupeane mikono na mtu aliye kando yako, kila upande, mbele yako, na nyuma yako, tunapouimba tena sasa.

Na . . . 

62-0714 Sauti Isiyojulikana
Open Bible Standard Church
Spokane, Washington Marekani

SWAHILI

©2024 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

Voice Of God Recordings
P.O. Box 950, Jeffersonville, Indiana 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org